




Sauti ya Siti

Toleo la 37

ISSN 0856 - 230 X

Agosti, 2015



Viti Maalum vyawagawa Watanzania

YALIYOMO

Ukurasa

Bukwimba: Niliitwa muuza baa, malaya, nikashinda jimbo	5
Wanawake wanaweza kupata asilimia 50 kupitia majimbo ya uchaguzi?	8
Ester Bulaya: Kujiamini kunaua uzalendo pofu wa wanaume....	11
Siri ya mafanikio ya usawa wa kijinsia katika Uchaguzi Mkuu	13
Wagombea urais wanawake wanaongezeka	15
Kwa nini Amina Salum Ali aligombea urais?	18
Viti Maalumu vyawagawa Watanzania	21
Wanawake wanabaki nyuma katika nafasi za juu za uamuzi	25
Vyombo vya habari vyabagua wagombea wanawake	28
Senkoro: Serikali itoe ruzuku kwa wagombea wanawake	31
Uwezekano wa Tanzania kupata Makamu wa Rais mwanamke	33

TAMWA



Sauti ya Siti

Mkurugenzi Mtendaji - TAMWA
Edda Sanga

Wahariri
Deodatus Balile
Lilian Timbuka

Usanifu
Gurnam Ajit

Chama cha Wanahabari Wanawake Tz
S. L. P 8981, Sinza - Mori,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2772681
Nukushi: +255 22 2772681
Barua Pepe: tamwa@tamwa.org

Ofisi za Zanzibar:
S. L. P 741, Tunguu,
Zanzibar, Tanzania
Simu: +255 773 747 252
B. Pepe: tamwazanzibar@tamwa.org

Tovuti: www.tamwa.org

TAHARIRI

CCM imeonyesha njia, vyama vingine pia viunge mkono wagombea wanawake

Oktoba 25 mwaka huu, Tanzania inafanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

Kimsingi, uchaguzi ni kiashiria muhimu kwa ustawi wa demokrasia katika nchi yoyote ile duniani.

Mara zote, uchaguzi ulio huru na wa haki huimarisha amani, umoja na uchumi wa nchi. Tayari tumeshashuhudia kuwa mara nyingi baada ya uchaguzi, serikali mpya zinazolingia madarakani, huja na sera mpya kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Tanzania ilipata uhuru wake mwaka 1961 na tangu wakati huo, imekuwa ikifanya uchaguzi huru na wa haki.

Mwaka 1965, Tanzania ilifuta mfumo wa vyama vingi na kuingia katika mfumo wa chama kimoja. Mabadiliko hayo yaliingiza mfumo wa chama kushika hatamu, mgombea mmoja wa kiti cha urais na wagombea wawili wa kiti cha ubunge na udiwani katika kila jimbo au kata.

Chaguzi ziliendelea kuwa huru na za haki hadi mwaka 1992 wakati mfumo wa vyama vingi uliporejeshwa. Kwa bahati mbaya katika mifumo yote miwili ya chama kimoja na vyama vingi, dhana ya usawa wa kijinsia haikutekelezwa.

Kutokana na kusahaulika kwa suala hilo, wanawake walishiriki katika uchaguzi wakiwa wapiga kura tu na watazamaji wa wagombea wanaume. ▶ Uk 4

CCM imeonyesha njia, vyama vingine pia viunge mkono wagombea wanawake

Dhana hiyo iliwanyima fursa ya kuchaguliwa katika ngazi za utoaji wa uamuzi ikiwamo ya urais, ubunge na udiwani. Tatizo kubwa hapa ni kuendelea kustawi kwa uzalendo pofu wa wanaume na mfumo dume ambao umejengeka zaidi katika nchi nyingi za Kiafrika ambazo jamii yake inawaona wanaume ndiyo viongozi pekee wa familia na jamii kwa ujumla.

Kutokana na jitihada za wanaharakati wa masuala ya jinsia kutaka usawa, kilio chao kikaanza kusikilizwa. Mwaka 1995, Serikali ya Tanzania ilianzisha viti maalumu vya ubunge na udiwani kama njia ya kuwajengea uwezo wanawake.

Pia, ni mwaka huohuo, Rose Lugendo alikuwa mwanamke wa kwanza kutangaza nia ya kutaka kuteuliwa kugombea urais kwa tiketi ya CCM. Mwaka 2005, idadi ya waliotangaza nia iliongezeka na kufikia watatu ambao ni Anna Senkoro (PPT-Maendeleo), Chiku Abwao na Maulida Komu kupitia CHADEMA.

Hakuna ambaye alichaguliwa. Katika ngazi ya majimbo mwaka 2010 ni asilimia tisa tu ya wanawake walioshinda ubunge.

Mwaka huu, idadi ya wanawake waliotangaza nia iliongezeka kwa chama tawala hadi kufikia saba.

Watangaza nia hao walikuwa ni pamoja na Balozi Amina Salum Ali, Dk. Mwele Malecela, Monica Mbega, Dk. Asha-Rose Migiro, Ritta Ngowi, Hellen Elinawinga na Veronica Kazimoto. Dk. Migiro na Balozi Amina walifika ngazi ya tatu bora.

Tunasema hatua ya wanawake wawili kufikia kwenye kinyang'anyiro cha tatu bora ni mafanikio makubwa kwa wanaharakati wa haki za binadamu na jinsia.

Pia, Dk. John Magufuli ambaye alishinda katika vikao vya uteuzi vya chama chake, alimteua Samia

Suluhu Hassan kuwa mgombea mwenza.

Hii ina maana kuwa kama Dk. Magufuli atashinda urais, kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania kutakuwa na Makamu wa Rais mwanamke.

TAMWA kwa kushirikiana na wanaharakati wengine wa jinsia na haki za binadamu wamekuwa wakipambana kuhakikisha kuwa wanawake wanashika nafasi za juu za utoaji wa uamuzi ikiwa ni pamoja na urais, umakamu wa rais na uwaziri mkuu.

Tuna imani kuwa huu ni mwanzo mzuri na tunatarajia kuwa vyama vingine vitaiga hatua hii ya kuwatambua wanawake ambao wana uwezo wa kushika nafasi kama hizi.

Toleo hili la Sauti ya Siti ambalo linafadhiliwa na Ford Foundation, linawapongeza wanawake ambao wamethubutu na kuwahamasisha wengine kujitokeza kwa wingi kushiriki kuchagua na kuchaguliwa katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani. Hii inatokana na imani kuwa wanawake wana uwezo sawa na walionao wanaume. ●

Uwakilishi wa wanawake na wanaume bungeni



64%



36%

Sauti ya Siti

Bukwimba: Niliitwa muuza baa, malaya, nikashinda jimbo

Na Beatrice Bandawe

Mwaka 2009, Jimbo la Busanda, mkoani Geita lilipoteza mbunge wake kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Faustine Lwilomba aliyefariki dunia nchini India alikokwenda kwa ajili ya matibabu.

Kwa taratibu za Sheria ya Uchaguzi, mbunge anapofariki dunia, uchaguzi mdogo huitishwa kuchagua mwingine atakayewakilisha wananchi wa jimbo husika bungeni.

Ni katika kipindi hicho, ndipo mwanamama Lolesia Bukwimba (44), alipojitosa kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi

mdogo wa jimbo hilo kupitia CCM.

Ingawa wanawake wengi huogopa kuingia kwenye uchaguzi wa jimbo kutokana na mikikimikiki ya kupambana na wanaume, Bukwimba alijipa ujasiri.

"Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kugombea kupitia jimbo. Nilijipa ujasiri kuwa wanawake tunaweza kama tukidhamiria," anasema Bukwimba ambaye kipindi hicho cha 2009 alikuwa na umri wa miaka 38 tu.

Katika uchaguzi huo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Umoja wa Demokrasia (UDP),

vilisimamisha wagombea na kufanya idadi ya wagombea katika uchaguzi huo kuwa wanne.

Bukwimba akiwa mwanamke pekee aliyejitosa katika uchaguzi huo, anasema kilichomfanya aingie kwenye kinyang'anyiro hicho ni maombi ya wananchi kumtaka agombe.

"Mwanzo niliona kazi ya siasa ni ngumu, lakini nilipoamua nikasema sasa nakwenda kugombea."

Matokeo ya uchaguzi yalipotangazwa, anasema aliongoza kwa kupata kura 29,242 na mpinzani wake wa karibu kutoka CHADEMA alipata kura 22,799 na hivyo kumzidi kwa kura 6,443.

►► Uk 6



Mbunge wa Jimbo la Busanda, Lolesia Bukwimba akiwahutubia wakazi wa kata ya Mgusu, jimboni humo wakati Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alipotembelea Mkoa wa Geita, Juni, mwaka huu



Bukwimba: Niliitwa muuza baa, malaya, nikashinda jimbo

Wakati anaamua kugombea ubunge wa jimbo hilo, mume wake alimpa ushirikiano mkubwa na hiyo ilimtia moyo pia.

“Kitendo cha kumshirikisha mume wangu katika uamuzi wangu wa kugombea jimbo na kunikubalia kilinipa moyo na nikajiona naweza,” anasema.

Kabla ya kuingia kwenye siasa, Bukwimba alikuwa anafanya kazi kwenye taasisi zisizo za kiserikali (NGO) na pia katika taasisi za kifedha.

Changamoto

Anasema jamii imezoea kuwaona wanawake kuwa ni watu dhaifu wasioweza kuongoza wanaume kutokana na mila na desturi zilizojengeka tangu enzi za mababu na mabibi.

“Kuna ile dhana iliyojengeka kwa baadhi ya wanaume kwamba mwanamke hawezi kuongoza wanaume, hiyo ilikuwepo kwenye jimbo nililokuwa nagombea,” anasema.

Kipindi alichokuwa kwenye kampeni, anasema wanaume aliokuwa akipambana nao walikuwa wakitumia silaha hiyo kuwashawishi wananchi wasimchague.

Anasema walikuwa wakimuita majina mengi ya kuudhi na

kukatisha tamaa na pia walisema haiwezekani watawaliwe na mwanamke.

“Waliniita mimi muuza baa, malaya na mengine mengi ya kunikatisha tamaa, lakini nilisimama imara sikutetereshwa na maneno yao.”

Anasema alipokuwa akisimama kwenye majukwaa ya kampeni kuomba kura, alikuwa hajitetei kwa kuwajibu wale waliokuwa wakimtukana, badala yake aliwaeleza nia yake ya kuwatumikia na kutoa mifano ya wanawake waliofanya vizuri katika uongozi wa kitaifa na kimataifa.

Aliwatajia wananchi hao wanawake kama Anne Makinda, ambaye ni Spika wa Bunge, Dk. Asha-Rose Migiro, ambaye alikuwa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa na sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Getrude Mongela, aliyekuwa Mbunge wa Ukerewe ambaye alifanya maendeleo makubwa katika jimbo hilo ambaye pia alishika nafasi mbalimbali za kimataifa na Profesa Anna Tibajuka, aliyekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat).

Mbali ya kushika nafasi mbalimbali nchini kwa mfano, Mongela pia aliweka rekodi ya kuwa spika/Mwenyekiti wa kwanza wa Bunge la Afrika.

“Vilevile, nilikuwa nikiwapa ile kaulimbiu ya ‘unapomuelimisha mwanamke, unaelimisha jamii nzima,’” anasema Bukwimba na kuongeza kuwa wananchi walihamasika na kumuelewa.

Rushwa

Wanawake wengi wanaogopa kupambana kwenye majimbo kutokana na uzoefu kuwa kwenye uchaguzi huo, wagombea hasa wanaume wenye uwezo hutumia fedha kununua wapiga kura.

Bukwimba anasema wanawake wanaonekana dhaifu kwa sababu ya kuchukuliwa kuwa hawana uwezo wa kifedha kushindana na wanaume.

Hata hivyo, yeye aliweza kushawishi wapiga kura kwa uzoefu wake wa kuzungumza na kutetea hoja zake, hali hiyo ilimsaidia na hatimaye alifanikiwa kuchukua jimbo.

Mbali na kushinda kwenye jimbo hilo, mwaka 2009 baada ya kifo cha mtangulizi wake, aliweza kulitwaa tena katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

Hivi sasa anajiandaa kulishikilia tena katika Uchaguzi Mkuu wa 2015.

▶▶ Uk 7

Vipaumbele katika jimbo

Alipoingia jimboni, kitu cha kwanza alichofanya ni kuangalia mahitaji muhimu ya wananchi.

Aligundua kuwa umeme, maji, elimu na barabara ndiyo kero kubwa katika jimbo hilo.

Anasema watoto wengi wa kike waliokuwa wakiandikishwa shule walikuwa hawamalizi masomo, hivyo kipaumbele chake cha kwanza kilikuwa elimu.

“Nilipita shule mbalimbali kuhamasisha wananchi umuhimu wa elimu, kwa sababu mimi pia nimesoma katika mazingira hayo hayo ya vijijini.”

Anasema alikuwa akiwaambia wazazi wawasomeshe watoto wao kwani kuna siku watakuja kuwa watu wakubwa kwenye nchi na kuwasaidia.

“Wananchi walihamasika, kuna wengine walidiriki kusema watasomesha watoto wao ili waje kuwa kama mbunge Bukwimba... Ilinipa moyo kwa sababu naamini siku za usoni watakuja kuleta mabadiliko,” anasema.

Pamoja na jitihada za kuhamasisha, alikuwa anatoa misaada katika shule za kata kama vitabu na katika shule 16 za sekondari za jimbo hilo alitoa kompyuta tano kwa kila shule alizoziomba kutoka kwa wafadhili.

Kutokana na jitihada zake za kusaidia wanafunzi aliwatafutia nafasi mbalimbali vijana 500 waliomaliza shule za sekondari katika kipindi chote cha ubunge wake na kati yao, 400 wamepata ajira.

Bukwimba: Niliitwa muuza baa, malaya, nikashinda jimbo



Aidha, kwa upande wa umeme, amesaidia kata tisa kati ya 16 zilizokuwa hazina nishati hiyo.

Ushauri kwa wanawake

Anawataka wanawake kuwa na ujasiri wanapotaka kufanya jambo lolote. Anasema hata kama kuna watu wanaowakatisha tamaa, wasiwasikilize kwa sababu watu wa aina hiyo hawapendi kuona maendeleo ya wengine.

“Wakati nilipokuwa naingia kwenye kinyang’anyiro cha jimbo, kuna wengine waliniambia sitaweza na kunishauri niende kwenye viti maalumu, lakini mimi nilishikilia msimamo wangu na ujasiri wangu ulinisaidia,” anasema.

Anawataka wanawake kutoogopa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwani wakisimama imara wana uwezo.

Anasema kuna wanawake wengi wenye uwezo nchini, lakini suala la kudhalilishwa kwenye majukwaa linawafanya washindwe kujitokeza kupambana na wanaume kwani hutumia udhaifu huo kuwatisha.

“Wapo wanawake waliosoma na wana uwezo mkubwa wa uongozi, lakini wanashindwa kujitokeza pengine kwa kutoamua au kuogopa, lakini hizo ni hisia tu, wakiwa na ujasiri wa kusimama na wanaume watawashinda.”

Anazungumziaje viti maalumu?

Bukwimba anasema, lengo la kuwekwa kwa viti maalumu ni kuwasaidia wanawake kupata jukwaa la kujifunza wanapokuwa ndani ya Bunge na kuwapa ujasiri wa kuweza kusimama wenyewe bila kutegemea uteuzi wa vyama.

Anasema kuna wanawake bungeni walioingia kwa tiketi ya viti maalumu lakini wana uwezo mkubwa wa kuchangia hoja na kutetea miko wa wanayotoka.

“Kuwa mbunge wa viti maalumu haina maana kuwa umebebwa, kwani hata kupata hivyo viti maalumu pia lazima upitie mchakato na kuna mikikimikiki kama ya kugombea kwenye majimbo.”

Bukwimba anasema mbunge wa jimbo anawajibika zaidi kwenye jimbo lake alilochaguliwa hasa anapokuwa anawakilisha wananchi wake bungeni, lakini wa viti maalumu anakuwa ni wa mkoa mzima anaotoka. ●

Wanawake wanaweza kupata asilimia 50 kupitia majimbo ya uchaguzi?

Na Elizabeth Edward

Miaka minne iliyopita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Kikwete alitia saini Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilifungua milango ya kuanza mchakato wa kutafuta Katiba Mpya yenye misingi ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mchakato huo ulianza kwa kuundwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilikuwa na kazi ya kukusanya maoni ya wananchi nchi nzima ili kuwapa fursa ya kuelezea mambo wanayotaka yawemo kwenye Katiba Mpya.

Miongoni mwa masuala yaliyokuwa yakipigiwa kelele ni usawa wa kijinsia katika masuala mbalimbali ikiwamo uwakilishi wa wananchi bungeni.

Dhana hii ya 50 kwa 50 ilikuwa ikisitiza kuwapo kwa idadi sawa ya wanawake na wanaume bungeni.

Kwa sasa kuna asilimia tisa pekee ya wanawake ambao wamepata nafasi hiyo kupitia majimbo na asilimia 27 iliyosalia wakiwa ni wabunge wa viti maalumu na wa kuteuliwa.

►► Uk 9



Wabunge wanawake wakiingia bungeni hivi karibuni mjini Dodoma

◀ Uk 8

Baada ya maoni ya wananchi na wajumbe wa Bunge Maalumu la Katiba kukusanywa, Katiba Inayopendekezwa ilikuja na azimio la kuwapa nafasi wanawake kwa kiwango cha asilimia 50 katika kila ngazi ya uchaguzi.

Swali linakuja baada ya Katiba Inayopendekezwa kukwama ilhali Uchaguzi Mkuu unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, wanawake wanaweza kujaza asilimia iliyobaki kupitia majimbo?

Mkurugenzi wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia (TGNP), Dk. Vicensia Shule anasema jambo hilo litawezekana endapo vyama vya siasa vitafungua milango na kuwapa nafasi wanawake ili washiriki kwenye kinyang'anyiro hicho.

Anasema hakuna njia nyingine itakayowezesha kuongezeka kwa idadi ya wanawake bungeni isipokuwa kupitia vyama vya siasa kwani hivyo ndivyo vyenye ridhaa ya kusimamisha wagombea katika nafasi mbalimbali.

"Vyama vingi vya siasa vinaongozwa na mfumo dume, haviwaamini wanawake kwa hofu ya kupoteza majimbo, vimejikita kwenye utamaduni unaoendelea kutoa nafasi kwa wanaume na kuwakandamiza wanawake," anasema Dk Shule.

Mwanaharakati wa kutetea haki za wanawake nchini, Anna Sangai anasema inawawia vigumu wanawake kujaza nafasi hiyo kupitia majimbo kutokana na mfumo wa vyama vya siasa hasa katika kufanya uteuzi wa wagombea.

Anasema vyama vingi vya siasa vinaamini kuwa wanaume ndiyo

Wanawake wanaweza kupata asilimia 50 kupitia majimbo ya uchaguzi?



wana nafasi kubwa ya kushinda kwenye kinyang'anyiro hivyo kuwanyima fursa hizo wanawake kwa kigezo cha udhaifu na nguvu.

"Binafsi naamini kiongozi awe rais au mbunge anaongozwa na

Katiba, lakini kwenye vyama vingi vya siasa bado wana ile dhana ya kuwa wanaume ndiyo wanastahili kuongoza kwa sababu ya nguvu, jambo linalowanyima nafasi wanawake," anasema Sangai.

Dk. Shule anasema kuna kila sababu ya wanasisa kuona haja ya Katiba Mpya iwe na kipengele kitakachoelekeza endapo Rais atakuwa mwanaume basi makamu wake au waziri mkuu awe mwanamke.

"Tunafahamu wanaume wana asili ya kupenda mamlaka, lakini suala hili linapaswa kuangaliwa kwa jicho pevu, ifike wakati wanawake washike nafasi za juu za uongozi wa nchi; hilo tutaendelea kulipigania siku zote.

"Kama nchi inaongozwa na katiba basi hata mwanamke anaweza kuchukua jukumu hilo bila wasiwasi, hakuna sababu inayoweza kutuweka kando kana kwamba uongozi ni kwa ajili ya wanaume pekee," anasema Dk Shule. ▶ Uk 10



Wanawake wanaweza kupata asilimia 50 kupitia majimbo ya uchaguzi?



Wakati wanaharakati hao wakionyesha hofu ya kushindwa kufikia lengo la 50 kwa 50 katika uwakilishi bungeni, baadhi ya wanawake wanaotarajiwa kujitosa katika Uchaguzi Mkuu ujao wamekuwa na mawazo tofauti.

Sada Kabezi ambaye ni mmoja wa wanawake waliojitosa kuwania nafasi ya ubunge katika Jimbo la Kaliua kwa tiketi ya Chama cha Maendeleo na Demokrasia (CHADEMA), anasema uadilifu na uchapakazi wake ndiyo unaomfanya ajiamini kuwa atapitishwa na kupeperusha bendera ya chama chake.

“Najiona wazi nikipata nafasi hiyo licha ya kuwa nashindanishwa na wanaume, lakini uwezo wangu ndani ya chama unafahamika.

“Ni mwanamke imara ambaye nimepania kuwakomboa kifikra wanawake wenzangu sambamba na kuleta maendeleo jimboni kwangu,” anasema.

Kwa upande wake, Jesca Kishoa anayewania kuteuliwa na NCCR-Mageuzi kugombea ubunge Iramba Magharibi, anasema kujitosa kwake kuwania nafasi hiyo kumetokana na uwezo alionao na anaamini jinsi yake haiwezi kuwa kikwazo kwa chama chake kushindwa kumpa ridhaa.

“Nitasimama kama mgombea, jinsi yangu haiwezi kuwa kikwazo naamini chama changu kitanipa nafasi kwa kuangalia uwezo na utendaji kazi wangu siyo jinsi,” anasema Kishoa.

Kauli za Kishoa na Kabezi hazipishani sana na kauli iliyotolewa na Ruth Mpangalala anayewania tiketi ya kugombea udiwani katika Kataya Buzurugwa iliyopo Ilemela jijini Mwanza kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Anasema kushiriki kwake katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye kata hiyo, kumemjengea imani kubwa kwa wananchi hata kufikia hatua ya kumshawishi kugombea nafasi hiyo.

“Wagombea tupo wengi lakini najipima kutokana na uwezo nilionao na ushiriki wangu katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye kata, naamini chama changu kitanipa nafasi.”

Naye Goodluck Temba, mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam anasema uwezo na jitihada zinazoonyeshwa na wanawake itakuwa moja ya chachu itakayowawezesha kufikia azma ya 50 kwa 50 katika ngazi za uongozi.

Anafafanua kuwa endapo mwanamke ataonyesha weledi na uwezo, ni vyema wananchi wakamchagua bila kuangalia jinsi yake.

“Binafsi sioni tatizo kumchagua mwanamke endapo ataonekana kuwa na sifa na uwezo kuliko mwanaume. Huo ni wito wangu hata kwa wanaume wengine tusiangalie jinsi, bali utendaji wa mtu,” anasema Temba.

Mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Daniel Kitwana anasema wanaume watakuwa tayari kushirikiana na wanawake kufikia dhana ya 50 kwa 50 endapo wataonyesha utayari na hali ya kujiamini.

Hakuna kitu muhimu ambacho wanawake wanapaswa kukizingatia kama kujiamini. Itawawia vigumu hata viongozi wa vyama kuyakata majina yao endapo watajitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu,” anasema Daniel Kitwana. ●



Ester Bulaya, mbunge wa viti maalum aliyekihama Chama Cha Mapinduzi Julai, mwaka huu na kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akihutubia wapiga kura mjini Bunda

Ester Bulaya: Kujiamini kunaua uzalendo pofu wa wanaume

Na Angela Kiwia

Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalumu kundi la vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mara, ambaye amehamia chama cha CHADEMA, ni miongoni mwa wabunge vijana waliochipukia na kuichachafya Serikali kutokana na kutokubaliana na baadhi ya mambo.

Namwalia Bulaya kwa jicho tofauti hasa kutokana na jinsi anavyojitanabaisha katika siasa huku akionekana kuwa na mwamko mkubwa wa kiuongozi

akiwa mwanahabari anayezidi kuchipukia katika siasa.

Mwandishi wa makala haya alifanya mahojiano na Bulaya ambayo

yalikuwa kama ifuatavyo:

Swali: Nini kinakupa hamasa ya kugombea nafasi ya ubunge wa jimbo?

Bulaya: Natambua kuwa hii ni haki yangu ya msingi kama haki nyingine za binadamu. Pia, jambo kubwa nikutaka kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Bunda kupitia Ubunge.

Pia ninataka kuwaaminisha kuwa wanawake wanaweza kutumikia nafasi ya ubunge bila kupitia viti maalumu.

Siyo kila mwanamke lazima awe mbunge wa viti maalumu.

Swali: Umekuwa ukikabiliana na ugumu upi katika siasa tangu uteuliwe kuwa mbunge?

Bulaya: Zipo changamoto kubwa katika Jimbo la Bunda na maeneo mengine nchini. Kwangu, naona kuna propaganda zaidi kwa wagombea wengi wanaume wanaotaka kuwaaminisha wapiga kura kuwa hawawezi kuongozwa na mwanamke. Huu siyo wakati wa kufanya propaganda chafu, bali tupimwe kwa ubora siyo kigezo cha jinsi kinachotumiwa na baadhi ya watu ili tu kumnyima mwanamke nafasi ya uongozi.

Swali: Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa inayoelezewa kutawaliwa na mfumo dume, utaweza kuuvunja?

Bulaya: Suala la mfumo dume katika Mkoa wa Mara lipo na lipo sana, ila ni lazima jamii ikubali kubadilisha fikra ili kuweza kuondokana na tatizo hilo.

Elimu lazima itolewe ya kutosha, namshukuru Mungu kuwa kwangu nimejitahidi kuhakikisha napunguza tatizo hilo katika Jimbo la Bunda, maana naitwa na wazee nazungumza nao jambo ambalo ni nadra sana. ▶ Uk 12





Ester Bulaya: Kujiamini kunaau uzalendo pofu wa wanaume

Kwangu hilo linanipa faraja na wapo watu wengi wananiunga mkono.

Swali: Familia yako inakuunga mkono au wapo baadhi wanaokubeza?

Bulaya: Namshukuru Mungu sana maana familia yangu pamoja na marafiki wote wananiunga mkono ikiwa ni pamoja na kukaa pamoja na kuzungumza jinsi ya kutatua changamoto zinazolikabili Jimbo la Bunda.

Swali: Nini ushauri wako kwa wanawake wengine nchini?

Bulaya: Wanawake ni lazima kujiandaa kisaikolojia, hii yote ni kutokana na jamii zetu kujaa woga, tunawaogopa wanaume. Iwapo hatutakuwa na woga tukashikamana, tutakuwa na ongezeko kubwa la wanawake katika vyombo vya uamuzi, pia wabunge wa majimbo.

Huu siyo wakati wa wanawake kukatishwa tamaa na kuwaogopa wanaume kwa kudhani kuwa wao ndiyo wanaofaa na wenye mamlaka nchini.

Swali: Ni changamoto zipi zilizo mbele yako na umejipanga vipi kukabiliana nazo?

Bulaya: Changamoto kubwa ni kutokujua nani unayegombea naye na amejipanga vipi kugombea na

watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha kuliko wewe, pia mfumo dume uliopo katika jamii yetu.

Suala la kujipanga kukabiliana nazo, nimeshaongelea hapo awali kwani Bunda ni nyumbani kwetu.

Hivyo pamoja na kutawaliwa na mfumo dume, tayari nimeshakutana na wazee na kuzungumza nao pamoja na vijana hivyo sina tatizo.

Swali: Je, umekwishafanya utafiti na kubaini nafasi yako ya kushinda ni kubwa kwa kiasi gani?

Bulaya: Katika suala la utafiti, ninaweza kusema nakubalika kwa wapiga kura maana kila nilichokifanya kinaonekana.

Bunda ni kama kulikuwa hakuna mbunge, nimekuwa mbunge wao wa kuteuliwa lakini nikifanya kazi kubwa kuliko mbunge wa jimbo.

Nimeweza kuwaunganisha vijana na kuanzisha kombe la Bulaya ambalo linazidi kuibua vipaji vya vijana wetu ikiwa ni pamoja na kuwakutanisha katika jimbo.

Suala la kushinda katika uchaguzi huo naamini kuwa chama changu kitafanya uamuzi sahihi, ila ninayo imani kuwa iwapo kitaniteua kugombea jimbo, ninao uhakika wa kushinda kwa kupata kura nyingi.

Swali: Unazungumzije uchaguzi wa mwaka huu na nafasi ya mwanamke?

Bulaya: Uchaguzi wa mwaka huu una changamoto kubwa, lakini ni lazima wanawake tutambue kuwa hakuna nafasi yenye mwenyewe, wapo wanawake wenye sifa zaidi ya hao wanaume waliojitokeza, hivyo ni jukumu letu kuendelea kuhamasisha wanawake kuendelea kujitokeza katika mwaka huu wa uchaguzi.

Jambo la kujivunia nikwa wanawake wengi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura tofauti na miaka ya nyuma. Hii inaonyesha namna walivyodhamiria kuijenga nchi yao.

Swali: Nini nafasi ya vijana nchini kuelekea Uchaguzi Mkuu ujao?

Bulaya: Mimi binafsi nimekuwa mstari wa mbele kupigania haki za vijana bila kuangalia itikadi zao za vyama, dini wala kabila.

Ni vyema wakatambua kwamba vijana wa Tanzania wakiungana na kufanya kazi kwa pamoja, hata kama watakuwa na itikadi tofauti za vyama, wataweza kulijenga Taifa lenye maendeleo na kujiamini. ●



Wanawake wamejiandikisha kwa wingi, swali pekee lililobaki ni iwapo wamehamasishwa kiasi cha kutosha kuchagua wanawake wenzao katika uchaguzi ujao

Siri ya mafanikio ya usawa wa kijinsia katika Uchaguzi Mkuu

Na Rachel Kyala

Misingi ya usawa wa kijinsia inapaswa kutambulika kama Tunu ya Taifa kwa kuwa itadhihirisha utashi wa nchi katika kutimiza maazimio ya kimataifa inayoyaridhia kuhusiana na masuala ya jinsia.

Utambuzi huo pia utaweka misingi ya kulijenga Taifa litakalojivunia usawa kati ya wanaume na wanawake kama mhimili muhimu wa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii bila kubaguana.

Jarida hili la Sauti ya Siti, hivi karibuni limezungumza

na baadhi ya watu waliotoa maoni yao kuhusu nafasi ya mwanamke katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwaka huu ambao wamezungumzia mitazamo yao.

Mkurugenzi wa Equality for Growth (EfG), Jane Magigita ambaye asasi yake

inajishughulisha na kazi ya kuwasaidia wafanyabiashara wasio rasmi hususan wanawake, anasema wanawake wana nafasi kubwa ya kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi bila woga, hususan kwa mwaka huu.

Magigita anasema ikilinganishwa na chaguzi zilizopita, mwaka huu wanawake wengi wamejitambua kuwa wana uwezo wa kuongoza na hawaoni sababu ya kuendelea kubaki nyuma.

Hata hivyo, akizungumzia mfumo wa siasa nchini anasema bado una kasoro licha ya wanawake kuonyesha kuhamasika.

Anasema bado nafasi ya mwanamke kushika uongozi katika ngazi mbalimbali inaminywa na mfumo dume ambao bado unaendelea kutawala licha ya kuanza kudhibitiwa.

“Bado katika maeneo mengi ile kasumba ya kuwa mwanamke hawezi kuwaongoza wanaume katika nafasi za ubunge, udiwani na urais, inagonga masikio ya walio wengi,” anasema Magigita.

Anasema hali hiyo ndiyo inayochangia asilimia kubwa ya wanawake kushindwa kusimama kwa miguu yao kutaka kuthubutu kuomba wananchi ridhaa ya kuwaongoza.

“Kwenye vyama vya siasa nako bado kuna changamoto, havijaweka mikakati zikiwamo sera na kanuni zinazomwezesha mwanamke kupata nafasi ya kuongoza,” anasema.

Anatolea mfano wa nafasi za ubunge akisema zina ushindani mkubwa katika kila uchaguzi, hivyo kuondoa fursa kwa wanawake kushiriki au kupata nafasi. ▶ Uk 14



“Nasema hivyo kwa sababu wengi wao wakijaribu kugombea kwenye ngazi ya jimbo hujikuta wakikumbana na vingi kutoka kwa wanaume ambao wamekamata fursa mbalimbali za uchumi,” anasema Magigita.

“Na hii inasababishwa na mfumo usio rasmi ambao umetawala mfumo wa uchaguzi ambao wagombea wengi huwekeza nguvu ya fedha ili waweze kuwashawishi wapigakura wawachague. Sasa wanawake wengi hawana fedha.”

Magigita anasema, ilani za uchaguzi pia hazilengi mahsusi kumwinua mwanamke kwani ahadi zipo lakini utekelezaji ni mdogo.

Hata hivyo, anasema wanawake wachache wanaobahatika kupata nafasi hizo nao wana tabia ya kung’ang’ania madaraka kwa muda mrefu pasipo kutoa fursa kwa wengine kugombea.

Anatoa mfano wa nafasi za viti maalumu kuwa wanawake waliopo madarakani hawaonyeshi utayari wa kuziachia ili kuwapisha wengine.

“Tabia ya kupokezana madaraka itawasaidia wanawake wengi kupata uzoefu wa kuongoza hasa katika nafasi ya ubunge na udiwani. Mtu akitoka hapo anakuwa na ujasiri wa kwenda kupambana jimboni na hata kuwania nafasi ya juu zaidi ya urais wa nchi,” anasema Magigita.

Anaonya wanawake kuacha tabia ya kubezana akiwataka waendeleo kutiana moyo ili malengo tarajiwa ya 50/50 yaweze kufikiwa katika ngazi za uamuzi.

Siri ya mafanikio ya usawa wa kijinsia katika Uchaguzi Mkuu



Mwandishi wa habari mkongwe nchini, aliyewahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya vyumba vya habari ikiwamo ya ukurugenzi wa iliyokuwa Redio Tanzania (TBC) na umeneja wa Mliman Radio na Televisheni, Edda Sanga anasema huu siyo wakati wa wanawake kubaki nyuma.

Akitoa maoni yake kuhusu mfumo wa siasa nchini na nafasi ya mwanamke katika kushika uongozi kwenye kada ya siasa, anasema jamii inatambua vyema kuwa mwanamke anaweza kuongoza kama akipatiwa nafasi. “Hii sisemi kwa kupapasa, bali nimeshuhudia mwenyewe nilipokuwa madarakani, waliokuwa wananibezwa ilifika mahali wakaikubali kazi yangu.”

Hata hivyo, anasema tatizo lililopo ni mfumo wa kukariri ulioitawala jamii kuwa, mwanamke akipatiwa madaraka, hawezi kuwaongoza kama mwanamume kwa madai kuwa hana ustahimilivu pindi

mambo yanapomzidia, jambo alilolipinga.

Anasema umefika wakati kwa asasi mbalimbali kuungana ili kutoa elimu kwa umma ifute dhana hiyo yenye mawazo mgando kuwa mwanamke hawezi kuiongoza jamii.

Sanga anasema Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), ambacho yeye ni miongoni mwa waanzilishi, kinaendelea kutoa elimu kila kona kwa lengo la kukomesha mfumo huo ambao unamgandamiza mwanamke kwa kumfanya aonekane ‘kibaraka’ ndani ya nchi yake.

“Mbali ya TAMWA, kuna asasi nyingi ambazo zimeendelea kuielimisha jamii juu ya athari ya mfumo dume. Tunashukuru kuona hivi sasa kuna mabadiliko makubwa, ndiyo maana mwaka huu wa Uchaguzi tunashuhudia wanawake nao wakithubutu kuomba ridhaa ya kuongoza nafasi nyeti ya urais.

“Lakini kuomba ridhaa tu haitoshi, tunataka wanawake hawa wapewe ushirikiano ndani ya vyama vyao na kwa jamii ambayo ina mamlaka ya kumchagua mtu wanayetaka awaongoze.

“Hapa ndipo penye changamoto kubwa, lakini binafsi ningeisihii jamii, iache kuwadharau wanawake wanaojitokeza, wawapatie ushirikiano wa kutosha kwa kuwaunga mkono ili nao wafikie ndoto zao.”

Anasema Tanzania ina idadi nzuri tu ya wanawake ambao ni viongozi katika ngazi za ukuu wa wilaya, mikoa na ukurugenzi, ingawa katika ngazi kubwa ikiwamo uwaziri, bado wako wachache. ▶ Uk 15

Siri ya mafanikio ya usawa wa kijinsia katika uchaguzi mkuu

“Tunaona ufanyaji wao wa kazi, hauna tofauti na wanaume na wapo wengine hata hao wanaume hawawapati. Jamii iache kuwabeza iwachague wawatumikie,” anasisitiza Sanga.

Mratibu wa Umoja wa Wanawake Wanasiasa Tanzania (Ulingo), Dk. Ave Maria Semakafu akizungumzia suala hili anasema, mfumo uliopo sasa hautoi fursa kwa wanawake kuingia katika uongozi, ingawa ukweli ni kwamba wenyewe wanapenda.

Anatoa mfano wa baadhi ya vyama vya siasa ambavyo hata katika Uchaguzi Mkuu ujao hasa kwa nafasi za ubunge, havijatoa fursa ya kuteua wanawake ili waingie kwenye kinyang’anyiro.

Anasema hali halisi inajionyesha pia hata katika kinyang’anyiro cha urais, mazingira hayaonyeshi kuruhusu wanawake kupata ujasiri wa kujitokeza na kuchukua fomu.

“Hali hiyo inatokana na baadhi ya wagombea wanaonekana kuwa na nguvu ambao inasemekana wanatumia gharama kubwa katika mikutano ya kutangaza nia, wengine wanatumia fedha nyingi kiasi cha kuwafanya wanawake waingiwe na woga,” anasema Dk. Semakafu.

Lakini, anasema hali hiyo isiwakatishe tamaa wanawake wote wenye nia ya kugombea nafasi kuanzia ngazi ya udiwani na ubunge.

“Wajitokeze kwa wingi, sisi tuko pamoja nao tutawajengea uwezo ili waibuwe na ushindi,” anasema Dk. Semakafu. ●



Dk. Asha Rose Migiro ni mmoja kati ya wanawake sita walioonesha nia ya kugombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM). Ingawa hakushinda, alifikia hatua ya tatu bora, ambapo Dk. John Magufuli ndiye alikabidhiwa bendera ya CCM katika uchaguzi ujao

Wagombea urais wanawake wanaongezeka

Na Leon Bahati

Tanzania ilianza kufanya Uchaguzi Mkuu wenye ushindani katika kiti cha rais mwaka 1995, baada ya kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Ushindani wa nafasi hiyo ulionekana kwenye sura ya ushindani kutokana na kushindaniwa na watu wengi tofauti na miaka ya nyuma ya mfumo wa chama kimoja, ambao alisimamishwa mtu mmoja ili apigiwe kura ya ‘ndiyo’ au ‘hapana’.

Mpaka sasa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya chaguzi nne na wagombea 25 walichuana katika kipindi hicho. Lakini ni wawili tu ambao waliibuka kuwa washindi hao ni Benjamin William Mkapa (1995 – 2005) na Jakaya Mrisho Kikwete (2005 – 2015).

Hii ni kusema kwamba, katika historia ya vyama vya siasa nchini, mwanamke aliyewahi kusimamishwa na chama kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mmoja tu, naye ni Anna Senkoro. ▶▶ Uk 16

Senkoro aliwania nafasi hiyo kupitia chama cha PPT – Maendeleo mwaka 2005 na alipata kura 18,783 sawa na asilimia 0.17 kati ya watu 11.4 milioni waliopiga kura. Alikuwa anamenyana na wagombea 10 na kushika nafasi ya nane.

Wanawake walioomba kupitia vyama

Kwa kawaida kabla ya wagombea urais kupitishwa, hupitia kwenye mchujo ndani ya vyama vyao.

Mchujo huo hutokana na wale waliojitokeza kuwania nafasi hiyo ndani ya vyama husika.

Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2010, uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanawake watatu walijitokeza kuomba wateuliwe na vyama vyao lakini hawakupenya. Hawa ni Rose Lugendo, Chiku Abwao na Maulida Anna Komu.

Rose Lugendo aliomba CCM imteue, lakini jina lake halikuweza kupenya miongoni mwa makada 10 walioomba nafasi hiyo.

Komu na Abwao waliomba tiketi ya kugombea urais kupitia CHADEMA mwaka 2005 lakini wakashindwa dhidi ya mwanamume pekee, Freeman Mbowe.

Mwaka huo, Anna Komu aliteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Mbowe baada ya aliyekuwa ameteuliwa kwenye nafasi hiyo kufariki dunia.

Uchaguzi Mkuu 2015

Mwaka huu, 2015, wanawake saba walichukua fomu kuomba CCM iwateue kugombea nafasi hiyo. Hao ni Balozi Amina Salum Ali, Dk Mwele Malecela, Monica

Wagombea urais wanawake wanaongezeka



Mbega, Dk. Asha-Rose Migiro, Ritta Ngowi, Hellen Elinawinga na Veronica Kazimoto.

Hata hivyo, pamoja na wanawake hao kujitokeza, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na makada 42 waliojitokeza ndani ya CCM.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Sophia Simba anakiri kuwa tatizo bado ni kubwa na umoja huo umekuwa ukiwahimiza wanawake wajitokeze kugombea.

Anasema umoja wao haujali vyama na uko tayari kuwa nyuma ya mtu yeyote anayeteuliwa na chama chochote cha siasa ili kumpa nguvu ya ushindi.

Kwa nini wanawake wengi hawagombea urais?

Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia CHADEMA, Chiku Abwao anaamini kwamba wanawake wanaona nafasi ya rais ni kubwa kiasi kwamba hawawezi kuimudu.

“Wanawake wengi nchini ni waoga kushika madaraka makubwa. Wengi wanaamini kuwa hawawezi kushika

madaraka hayo makubwa katika nchi,” anasema Abwao.

Anasema: “Kabla mwanamke hajagombea nafasi kama hiyo, lazima ajiulize maswali mengi. Atajiuliza, je, kuna mwanamke aliyewahi kuwa waziri mkuu? Je, kuna mwanamke aliwahi kuwa makamu wa rais? Anapopata jibu la ‘hapana’, basi hujikuta akikata tamaa na kurudi nyuma.”

Mbega anasema urais ni nafasi ambayo ipo katika ushindani wa watu wengi wenye sifa tofauti.

Anakiri kuwa mwanamke kugombea nafasi ya urais lazima atakumbana nachangamoto nyingi zikiwamo za mfumo dume lakini anaamini kuwa Watanzania kwa sasa wameelimika na wako tayari kuongozwa na mwanamke mwenye sifa.

Kuhusu changamoto ambazo anaweza kukabiliana nazo kwenye kinyang’anyiro hicho, Mbega anasema katika chaguzi zote kuna ushindani mkubwa, lakini haumkatishi tamaa atasonga mbele.

» Uk 17



Anna-Mghwira- Mwenyekiti na Mgombea wa Urais kwa Tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo

« Uk 16

Wagombea urais wanawake wanaongezeka

Anatoa mfano namna alivyopambana katika uchaguzi wa ubunge Jimbo la Iringa mjini mwaka 2010 ambao hata hivyo hakushinda.

Anasema: "Katika uchaguzi ule tulipishana kwa kura 800 na mbunge aliyenishinda, ni jambo la kujivunia japo sikushinda, lakini nilipambana na mwanamume."

Balozi Amina Salum Ali, anasema Tanzania ina wanawake wengi wanaoweza kugombea urais, lakini hawajitokezi kwa hofu na imani potofu kuwa ni nafasi inayohitaji kuwa na fedha nyingi ili kuiwania.

"Wanaogopa kujitokeza wakihofia kugombea nafasi za juu za uongozi wanawake wengi wanaishia kuwa wanyonge. Lakini mimi nasema siyo kweli. Wajitokeze kwa wingi ili kutoa mchango mkubwa walionao kwa taifa letu."

Mwenyekiti wa Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Penina Mlama anasema Tanzania ina wanawake wengi wenye uwezo wa kuongoza ila kwa kuwa hakuna historia hiyo katika jamii, inawezekana ikawa jambo hili likaonekana kuwa haliwezekani katika nafasi ya urais.

"Kuna nchi kama Liberia na Brazil, hizi zinaongozwa na marais wanawake na wanafanya vizuri. Sisi pia tuna wanawake wenye uwezo wa kuongoza, sioni shaka yoyote," anasema Mlama.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, Deus Kibamba anasema kuna tatizo la miaka mingi la kimfumo ambalo linawafanya wanawake

hadi wasubiri wanaume waseme ndipo wafanye jambo.

Tatizo jingine anaeleza ni la rasilimali kwa maana kwamba wanaume ndiyo wanamiliki sehemu kubwa ya uchumi.

Kutokana na hali hiyo, Kibamba anasema wanaume wanakuwa na uwezo mkubwa wa kifedha hivyo kuwafanya wanawake waendeleo kuwa wanyonge na wazito kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa.

Ili kuondokana na hali hiyo, Kibamba anapendekeza Taifa kuweka kanuni kwamba Rais akiwa mwanamume, makamu awe mwanamke na hali hiyo iwe hivyo hata kwenye nafasi za juu katika uongozi wa vyama vya siasa.

Anasema hiyo itasaidia kuwahamasisha wanawake kujitokeza kwa wingi na itawaondolea ile hali ya kujiona kuwa wao ni wanyonge na hawastahili kuingia katika ushindani wa nafasi za uongozi ikiwamo ya urais. ●



Kwa nini Amina Salum Ali aligombea urais?

Amina Salum Ali ni waziri mstaafu na kwa sasa ni Balozi wa Umoja wa Afrika (AU) nchini Marekani. Alijitokeza akiwa mmoja wa makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliochukua fomu za kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Oktoba mwaka huu, akiwaomba wenzake kumuunga mkono. Mwandishi Wetu, DEOGRATIAS MUSHI alihojiana naye juu ya matarajio yake kisiasa na alikuwa alilenga kufanya nini ikiwa angefanikiwa kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Tanzania.



Balozi Amina Salum Ali akionesha fomu ya kuwania urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kuipokea kutoka kwa Katibu wa Oganizesheni wa chama hicho Mohamed Seif Khatib akiwa makao makuu ya Chama Cha Mapinduzi Dodoma, Juni mwaka huu. Kulia ni Anna Abdallah, Mwenyekiti wa zamani wa UWT.

Swali: Nini kimekusukuma kugombea urais?

Jibu: Wito wangu wa kufanya kazi na wanawake kuboresha maisha yao ndicho kimenisukuma kuomba fursa ya kutumikia ofisi kuu hapa nchini. Nimekuwa mwanasiasa nikiwa binti mdogo. Nimesafiri mno katika maeneo mbalimbali ya nchi hii yote Bara na Visiwani, nayafahamu vyema matatizo yanayowakabili kina mama.

Wanasema 'ukimwelimisha mwanamke moja kwa moja unakuwa umeelimisha taifa zima'.

Wanawake wengi katika nchi hii wanasaidia familia zao na wakipewa fursa nzuri za uchumi, nina uhakika wataiboresha jamii yote.

Wanawake na watoto ni kati ya makundi yaliyoachwa nyuma kimaendeleo. Nataka kubadili mwelekeo, kuwezesha wanawake wengi kushiriki shughuli za kiuchumi kama kilimo, biashara na vyanzo vingine vya kuzalisha mapato.

Swali: Unaacha ofisi kubwa jijini Washington DC kugombea urais. Kwa nini?

Jibu: Nchi yangu Tanzania inakuwa kipaumbele cha kwanza linapokuja suala la ningependa kufanya nini maishani mwangu. ▶▶ Uk 19

Kwa nini Amina Salum Ali aligombea urais?

Nimeitumikia Afrika, lakini wema huanzia nyumbani. Ningependa watu wangu, hasa wanawake kupata hali bora ya maisha.

Naipenda nchi yangu na nipo tayari kuitumikia kwa njia yoyote ambayo inaweza kuboresha maisha ya watu wetu.

Swali: Unadhani ni matatizo yapi makubwa yanayowakabili wanawake nchini kwa sasa?

Jibu: Niruhusu kwanza niwashukuru marais wetu wanne walioongoza nchi hii tangu tupate uhuru. Wamefanya kila wawezalo kuboresha hali za wananchi.

Rais Jakaya Kikwete amefanya mengi kuboresha miundombinu na pia amewateua wanawake kuwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wabunge na pia makatibu wakuu katika wizara mbalimbali.

Hata hivyo, wanawake Tanzania kwa sasa wanakumbana na matatizo mengi ikiwamo bei ndogo za bidhaa zao sokoni, jambo linalowazuia kupata mbolea na zana nyingine kwa msimu unaofuata.

Hii inatokana na wanaume kumiliki uchumi katika familia ina maana kina mama hawawezi kusimama peke yao, hali inayowafanya kushindwa kufanya uamuzi juu ya mambo yao, siyo

katika kilimo tu, bali hata katika maisha yao.

Tanzania ya leo mwanamke mwenye njaa hajiamini na hana uwezo wa kudai haki yake.

Tumesikia mara kadhaa kesi za ukatili wa kijinsia zinazoishia katika ngazi ya familia wakiogopa kumfunga mleta mkate katika familia.

Kwa maana huyo akifungwa, maisha ya familia pia yanakuwa yamefungwa katika shida zaidi.

Mwanamke mwenye njaa pia hawezi kuwa na ziada ya kupanda daladala au pikipiki kutafuta haki yake mahakamani kwa kusafiri mamia ya kilomita kutoka nyumbani kwake.

Lililo bora kwake si kutafuta kumfunga mume wake aliyemfanyia ukatili, bali kuokoa maisha ya watoto wake wanaokufa njaa.

Mapambano ya kisiasa yameleta mafanikio yanayoonekana.

Anasema angependa kuona wanawake wanapata huduma bora za afya na pia wanapata huduma za jamii kama maji jirani na makazi yao.

Hayo yote yanawezekana ikiwa tutaweka mbinu sahihi za kumkomboa mwanamke.

Swali: Baadhi ya watu wanadhani muda wa mwanamke kuwa Rais wa Tanzania haujawadia. Unawaambia nini?

Jibu: Mimi nadhani huu ni muda mwafaka kwa mwanamke kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi hii. Tunapaswa kuacha mawazo ya kizamani, yaliyopitwa na wakati.

Tuna uzoefu mzuri ajabu wa kujifunza kutoka Brazil, Ujerumani na Liberia ambako wanawake wamefanya maajabu katika kuimarisha uchumi wa nchi zao.

Hatupaswi kuangalia jinsi linapokuja suala la uongozi wa nchi. Muhimu ni uwezo, uzoefu na kukubalika.

Nina uhakika nina kila sifa inayotakiwa kuongoza nchi hii nzuri. Nalifahamu taifa hili vizuri sana na ninakishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kilichonizawadia fursa za uongozi.

Nikiwa mwanamke Balozi wa kwanza wa Umoja wa Afrika, nimeazimia kuboresha haki za wanawake na masuala ya watoto.

Mimi ni mwanzilishi wa Taasisi ya Kushughulikia Masuala ya kina mama Zanzibar, inayolenga kupambana na masuala ya afya kwa wanawake na watoto.

Kama mbunge wa muda mrefu, nimeshika nafasi kadhaa za uwaziri katika Serikali ya Tanzania. Nafasi ya hivi karibuni ni ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

Nimekuwa mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Benki ya Kiislamu kwa Maendeleo ya Wanawake na nimekuwa mjumbe wa bodi mbalimbali ikiwamo ya Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro.

Zaidi ya hayo, nimeanzisha taasisi kadhaa za kuwajengea uwezo wanawake, ikiwamo Mfuko wa Rais wa Kujitegemea.

Nina shahada ya kwanza katika uchumi na MBA (Masoko). Watu wasiwe na wasiwasi hata chembe juu ya sifa zangu za uongozi.

▶▶ Uk 20

Nimesoma na kufanya kazi ndani na nje ya nchi, ninayo maarifa ya kutosha ya uongozi bora.

Swali: Unawazungumziaje wagombea wenzako ndani ya CCM?

Jibu: Nimekuwa nikifuatilia hotuba zinazotolewa na wagombea urais wenzangu kwa umakini na nimekatishwa tamaa kwamba hawazungumzii masuala ya wanawake wala kutamka ni kitu gani watawafanyia wanawake Watanzania kama watafanikiwa kupatiwa dhamana ya uongozi.

Huwezi kuzungumzia mapambano dhidi ya rushwa bila kuzungumzia haki za wanawake na watoto. Ningependa kusikia watapambanaje kuleta usawa wa kijinsia na fursa bora za kiuchumi kwa wanawake.

Swali: Utawezaje kuboresha uchumi wa nchi ikiwa utachaguliwa?

Jibu: Tanzania imejaliwa baraka nyingi zinazoiwezesha kuboresha uchumi wake.

Mlima mrefu kuliko yote Afrika wa Kilimanjaro upo Tanzania.

Vivutio vizuri vya watalii kama Ngorongoro Crater, Olduvai Gorge na Serengeti vinaweza kuzalisha fedha nyingi za kigeni.

Ardhi bora kubwa tuliyonayo inaweza kuboresha maisha ya wananchi ikitumika vyema. Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara vinaweza kuwa vyanzo vizuri ya mapato.

Gesi iliyogundulika hivi karibuni na mafuta, pia vinaiweka nchi katika nafasi nzuri ya kuboresha uchumi wake.

Kwa nini Amina Salum Ali aligombea urais?



Pia, tunapaswa kubadili fikra zetu kama taifa, ili kuhakikisha tunafungua viwanda vingi hapa nchini vitakavyozalisha bidhaa mbalimbali tunazozihitaji badala ya kutumia fedha kidogo za kigeni tulizonazo kuagiza bidhaa.

Kwa sasa bidhaa nyingi tunazotumia zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Mazao yetu ya shambani yanaweza kupata bei nzuri ikiwa yatachakatwa.

Kilimo chetu kinapaswa kuelekezwa katika viwanda. Kaulimbiu kama 'Isaidie Tanzania, Nunua Bidhaa za Tanzania' inapaswa kupigiwa chapuo kuanzia ngazi ya chini.

Tunapaswa pia kuboresha zaidi miundombinu ya nchi, viwanda, mawasiliano na njia za usambazaji ili kuwezesha rasilimali za nchi kufikiwa zaidi na kuvutia wawekezaji wa kigeni.

Tukivutia uwekezaji wa kigeni nchini, kampuni za kigeni zinaweza kuwekeza kwa wafanyakazi wa ndani.

Kampuni za kigeni zinaweza kutoa mafunzo na kusomesha nguvu kazi ya hapa nchini na kuajiri. Hii itatengeneza ajira na kuleta fedha zaidi katika uchumi wa nchi yetu.

Tuache kuuza nje malighafi na kuagiza bidhaa sizizo muhimu kutoka nchi zilizoendelea.

Swali: Nini mtazamo wako katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?

Jibu: Kama kuna lulu tunayopaswa kuiona kama hazina na kuitetea ni Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika.

Ingawa waasisi hatuko nao tena, wametuachia Taifa moja.

Tanzania ya mwaka 1964 imepitia mabadiliko makubwa kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda vyama vingi kuendana na mfumo wa kijamii na kiuchumi wa dunia na makubaliano ya kisiasa.

Watanzania wanajivuna kuwa na Muungano wa dola huru mbili uliotajwa na wengi kuwa wa pekee barani Afrika, kwani hakuna nchi yoyote iliyoiga mfano wa nchi hizi.

Watanzania hawajakatishwa tamaa na nchi nyingine za Afrika ambazo hazikuonyesha nia ya kuunda muungano mkubwa sawa na huu.

Chini ya Hati ya Makubaliano ya Muungano ya Mwaka 1964, mambo ya Muungano yaliyokubaliwa yalikuwa 11, lakini sasa ni zaidi ya 23. ▶ Uk 22



Wabunge wakiwa katika ukumbi wa Bunge mjini Dodoma hivi karibuni. Wapiga kura wanahamasishwa kuchagua wanawake wengi kuingia katika chombo hiki cha kufanya uamuzi

Viti Maalumu vyawagawa Watanzania

Na Reuben Kagaruki

Tanzania ipo kwenye mchakato wa kufanya Uchaguzi Mkuu wa rais, wabunge na madiwani ifikapo Oktoba 25, mwaka huu. Kwa sasa wanasisia wengi kutoka vyama mbalimbali wameanza kampeni ya kugombea nafasi hizo.

Katika kipindi hiki, Watanzania wengi wamekuwa na mtazamo tofauti kuhusu nafasi ya viti maalumu kwa upande wa wanawake katika ngazi za udiwani na ubunge na kuna mgawanyiko wa wazi.

Wengi wamekuwa wakikosa utaratibu unaotumika kuwapata, wakidai umegubikwa na

upendeleo wa kidini, ukabila, rushwa na hata unyanyasaji wa kijinsia (kingono).

Akizungumzia utaratibu unaotumika kupata wabunge na madiwani wa viti maalumu, Ofisa Uchaguzi wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Abdulrahman Lugone anasema chama hicho kinatumia mwongozo na utaratibu wa uchaguzi kwa mujibu wa katiba na kanuni za chama hicho.

Anasema mwongozo huo uliopitishwa na Kamati ya Utendaji Taifa na Baraza Kuu, una ratiba ya kura za maoni ndani ya chama ambayo inaonyesha tarehe ya uchukujaji na urejeshaji wa fomu, ratiba ya kura za maoni, usimamizi wa kura za maoni pamoja na uchujaji wa wagombea kwa mujibu wa katiba yao.

Anataja vigezo vinavyotumiwa na kamati za uchaguzi za majimbo na wilaya kuwapata wagombea wa ubunge wa jimbo, viti maalumu na madiwani kuwa ni pamoja na walioonyesha kuthubutu kwa kujitokeza kugombea.

Anasema itakapotokea wakashindwa katika kura za maoni, wanakuwa wamepata sifa ya kuingizwa katika kinyang'anyiro cha viti maalumu hata kama hawakujaza fomu za kuomba kuwania nafasi hizo.

Kwa wilaya zenye majimbo zaidi ya moja baada ya kamati ya uchaguzi ya kila jimbo kuwapanga wagombea udiwani wa viti maalumu waliopitishwa katika kata zao kwa mujibu wa vigezo, Kamati ya Utendaji inakaa na kuunganisha madiwani wa majimbo yote kwa uwiano sawa bila kupitia tena vigezo vyao.

Kwa upande wa wabunge wa viti maalumu, anasema Baraza Kuu ndilo lenye uamuzi wa mwisho wa kuwapitisha, lakini wanazingatia ukanda kutokana na idadi ya viti vya majimbo ambavyo chama kimeshinda.

Kuhusu kuwapo kwa hisia za wanawake kupewa viti maalumu kwa misingi ya upendeleo, udini, ukabila umajimbo na udhalilishaji wa kijinsia, Lugone anasema hilo haliwezekani. ▶ Uk 23



Kwa nini Amina Salum Ali aligombea urais?



Juhudi nyingi zimefanywa kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki, lakini majadiliano ya karibuni kati ya wakuu wa nchi tatu za Afrika Mashariki inaonekana siyo rahisi kuanzisha shirikisho la kisiasa.

Watetezi wa Muungano wamejenga hoja kwamba uchumi wa Zanzibar hauwezi kusimama peke yake kwani unategemea kwa kiasi kikubwa karafuu inayoweza kushuka bei muda wowote.

Kwa jicho la kiuchumi, shughuli za kibiashara zimeongezeka kati ya pande mbili za Muungano na watu wamenufaika.

Watu kutoka Bara wanasafiri kwenda Zanzibar kununua bidhaa na Wazanzibari wanakwenda Bara kwa shughuli za kibiashara.

Mafanikio ya wazi ya Muungano ni kwamba umedumu kwa muda mrefu kuliko Muungano wa aina yoyote kwa Afrika.

Licha ya upungufu mwingi, Muungano wa Tanzania ni mfano unaong'ara wa kuunganisha watu wa mataifa huru mawili.

Faida kubwa ya Muungano ni kuwa, umewahakikishia usalama Watanzania na umepunguza vitisho kutoka nje.

Hivyo tuna kila sababu ya kuulinda Muungano huu kwa gharama yoyote.

Swali: Marafiki zako katika safari ya Ikulu wanatajwa kuwa na fedha. Wewe una nini?

Jibu: Sina fedha na sidhani kama nafasi za kisiasa zinapaswa kununuliwa.

Ninao wafuasi nyuma yangu walioamua kuniunga mkono. Ninamshukuru Anna Abdallah aliyeniunga mkono tangu siku ya kwanza nilipotangaza nia ya kuwania urais.

Nawaomba wanawake wengine kuniunga mkono katika safari hii ndefu.

Swali: Unalo neno kwa vyombo vya habari vya hapa nchini?

Jibu: Navishukuru vyote, magazeti na vyombo vya kielektroniki vilivyoandika habari zangu, ingawa havijaniweka katika kurasa zao za mbele. Kadiri muda unavyokwenda, nadhani watapaswa kutambua kwamba mimi ni mgombea bora anayekwenda kuokoa mama zao, dada, watoto na kila awaye katika jamii. ●



Balozzi Amina Salum Ali

Sauti ya Siti

Anasema kinachowezezana ni kutoa rushwa ya fedha wakati wa vikao vya kura za maoni.

“Mgombea anaweza kutoa fedha kwa wajumbe, lakini siyo mambo mengine.”

Katika ngazi ya ubunge, Lugone anasema ni ngumu kuwapa kwa chembechembe za vitendo vya rushwa wala vya udhalilishaji kwani Baraza Kuu lina wajumbe wasiopungua 60 kutoka kila mkoa akiwamo mwenyekiti wa chama na ndilo lenye uamuzi wa mwisho.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Temeke, Salama Masoud anasema mfumo huo ni mzuri, lakini baadhi ya viongozi wanakiuka kanuni na utaratibu uliowekwa na kusababisha kuwapa kwa vitendo vya rushwa.

Masoud anasema alijitokeza kugombea ubunge kupitia jimbo, lakini alikwamishwa na mgombea mmoja aliyeshinda katika kura za maoni kutokana na kutumia kila mbinu zikiwamo za rushwa.

Anasema mgombea huyo alitoa fedha kwa wajumbe na wakati mwingine alikuwa akimwambia kuwa yeye ni mwanamke, hastahili kugombea jimbo.

Masoud anasema aliamua kugombea nafasi ya udiwani, lakini nako alishindwa kutokana na wagombea wanaume ambao alikuwa akichuana nao kutoa rushwa.

“Nilipambana na wanaume kuomba ridhaa ya chama changu ili kiniteue kuwa mgombea udiwani niliangushwa na watu wachache waliokuwa wakitoa fedha kwa wajumbe kati ya Sh 50,000 hadi Sh100,000,” anasema Masoud.

Viti Maalumu vyawagawa Watanzania



Mbunge wa Viti Maalumu Rufiji, Kuruthumu Mchuchuri anasema kwa ngazi ya ubunge wa jimbo na viti maalumu ndani ya CUF, wameweka mfumo mzuri ambao unawabana watu wanaotaka kutumia rushwa.

Anasema kutokana na kuridhika na mfumo huo, amepitishwa na CUF kwenye kura za maoni kugombea ubunge Jimbo la Rufiji.

Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, Hussein Ramadhan anasema baadhi ya vyama vinatumia nafasi ya viti maalumu kudhalilisha wanawake.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Nape Nnauye anasema CCM inatenda haki katika kupata wabunge wa viti maalumu.

Anasema utaratibu ukiwa wazi, hakuna upendeleo unaofanyika katika nafasi hizo.

Akizungumza na Sauti ya Siti katika mahojiano maalumu, Nape anasema: “Utaratibu ndani ya CCM wa kupata wabunge

wa viti maalumu unafahamika na unasimamiwa na wanawake wenyewe, hivyo siyo rahisi ukawa na vitendo vya udhalilishaji.

“Kanuni ziko wazi, zinaelekeza na kila anayeomba nafasi hiyo anachaguliwa na wanawake wenzake.

“Hivyo chama kinasimama katika misingi ya kutenda haki na hakuna kitu kinachoamriwa nje ya kanuni na katiba ya chama katika kupata wabunge wa viti maalumu.”

Alipoulizwa madai ya kuwapa kwa rushwa ya ngono kwa wanaotaka nafasi hizo, Nape anasema: “Madai hayo hayana ukweli wowote, anayeomba nafasi hizo anachaguliwa kwa mujibu wa kanuni na utaratibu.”

Kwa upande wake aliyekuwa, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Zainabu Vullu anasema utaratibu wa chama kupata wabunge na madiwani wa viti maalumu unasimamiwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT).

▶▶ Uk 24

Anasema kutokana na uteuzi wao kusimamiwa na wanawake, hakuna uwezekano wa mtu kuchaguliwa kwa rushwa, udhalilishaji wa kingono wala ukabila.

Vullu anasema utaratibu wa kupata madiwani na wabunge wa viti maalumu ndani ya CCM unahusisha wanawake peke yao, hivyo hauna misingi yoyote ya udhalilishaji wa kijinsia (kingono).

“Tena sisi tukiona kuna mwanamume anashadadia (kushabikia) mchakato wa kuwapata wabunge wa viti maalumu basi tunasema aje tumshonee gauni na avae sidiria ili aweze kushirikiana na sisi,” anasema na kuongeza kuwa hiyo inaonyesha ni jinsi gani wao wanavyoshiriki kuamua mambo yao.

Anasema mchakato wa kuwapata wabunge wa viti maalumu ndani ya chama hicho unaanzia kwenye wilaya, mkoa hadi Taifa na wao ndiyo wamekuwa wakichagua.

Viti Maalumu vyawagawa Watanzania



Anasema wale wanaoshinda ndiyo wanaobaki kusubiri idadi ya wabunge ambao chama kitapata kupitia majimbo ili kupata asilimia inayotakiwa ya wabunge wa viti maalumu.

Anasema hata kwenye madiwani wa viti maalumu, mchakato wao unaanzia kwenye matawi ukihusisha wanawake peke yao.

Vullu anasema anakubaliana na mfumo wa uteuzi kwani ni mzuri.

Alipoulizwa kama ana mpango wa kuwania ubunge kupitia jimbo, alisema kwa mwaka huu hatafanya hivyo.

Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Naomi Kaihura anasema umefika muda kwa wanawake kupambana na wanaume kugombea ubunge kupitia majimbo.

Anasema nafasi za viti maalumu zinatoa fursa kwa wanaume na jamii kuwanyanyasa.

Akizungumza akiwa mkoani Dodoma, Kaihura anasema hawakubaliani na mfumo uliopo kwa wabunge wa viti maalumu kutopewa fedha za mfuko wa jimbo kama inavyofanyika kwa wabunge wa majimbo. “Wabunge wa viti maalumu tunanyanyasika bungeni ndiyo maana hata fedha za mfuko wa jimbo hatupatiwi,” anasema.

Kwa upande wa Chadema, anasema wabunge wa viti maalumu wanapatikana kwa kukidhi vigezo vilivyowekwa na chama na hakuna misingi ya udhalilishaji, rushwa wala vitendo vingine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wajasiriamali (Ashata), Lightness Lwekiza anasema wabunge na madiwani wa viti maalumu hawatendewi haki kwa kuwa wananyimwa fedha za mfuko wa jimbo.

Anasema wabunge hao wanafanya kazi kubwa kuliko wabunge wa majimbo. Lwekiza anasema siyo kweli kwamba wanapatikana katika mazingira ya udini, ukabila au rushwa ya ngono. ●



Wanawake wanabaki nyuma katika nafasi za juu za uamuzi

Na Nuzulack Dausen

Wakati joto la Uchaguzi Mkuu likizidi kupanda, ushiriki wa wanawake katika tukio hilo ni moja ya maeneo yanayotazamwa kwa jicho la karibu kutokana na historia ya jamii hiyo kuwa nyuma katika nafasi mbalimbali za uamuzi.

Uchaguzi wa kwanza baada ya kurudishwa vyama vingi mwaka 1995, ni asilimia 16 tu ya wagombea wote walikuwa wanawake. Wanawake wanane pekee walishinda viti vya ubunge majimboni huku 37 wakitoka Viti Maalumu na kufanya idadi yao kuwa 45 dhidi ya wabunge 269 waliochaguliwa.


Kadrisiku zinavyokwenda, idadi ya viongozi wanawake inaongezeka kwa wastani katika vyama vya siasa, bungeni na Baraza la Mawaziri tofauti na mwaka 1995, 2000 na 2010 kutokana na sera, mikakati na utashi wa Rais Jakaya Kikwete katika kuongeza nafasi ya wanawake katika jamii.

Wabunge wanawake wameongezeka kutoka asilimia 16 mwaka 1995 hadi 36 mwaka huu, shukrani kwa viti maalumu kwani idadi ya wanaochaguliwa majimboni inachehemea huku uchaguzi wa mwaka huu ukitumainiwa kuleta mageuzi makubwa.

Takwimu zilizotolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Sophia Simba wakati

akiwasilisha bajeti yake hivi karibuni bungeni, zinaonyesha kuwa idadi ya wabunge wanawake imeongezeka kutoka 62 kati ya wabunge 288 mwaka 2005, hadi kufikia wabunge wanawake 127 kati ya 357 mwaka 2015.

Hata hivyo, idadi hiyo imechangiwa na nafasi nyingi za viti maalumu ambazo hutegemea majaliwa ya kiwango cha wabunge waliochaguliwa katika majimbo kwenye Uchaguzi Mkuu na uteuzi wa Rais. ▶ Uk 26



Ukilinganisha na nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania imejitahidi kwa nafasi ya mwanamke katika uongozi ikiwa nyuma ya Rwanda ambayo ndiyo inayoongoza ulimwenguni kwa kuwa na zaidi ya asilimia 50 bungeni.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mabunge Ulimwenguni (IPU), Uganda inafuatia baada ya Tanzania ikiwa na wabunge wanawake 135 kati ya 386 baada ya Uchaguzi wa Februari, 2011.

Uwiano baina ya wabunge wanawake nchini Burundi umezidi kushuka na IPU inaonyesha kuwa hadi wakati Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 ulipofanyika, Bunge la nchi hiyo yenye watu takriban milioni 10.5 lilikuwa na wabunge wanawake kwa asilimia 32.


Nchini Kenya, hali siyo nzuri sana katika Bunge la Taifa kwani idadi ya wabunge wanawake ni asilimia 19 baada ya Uchaguzi Mkuu wa Machi, 2013 kutoka asilimia 10 baada ya uchaguzi uliotawaliwa na vurugu wa mwaka 2007.

Uwepo wa idadi kubwa ya wabunge siyo kipimo pekee cha mafanikio ya uwezeshaji wanawake iwapo nafasi za juu zikaendelea kukaliwa na wanaume kwa asilimia kubwa. Lakini ndani ya nchi za ukanda huo, hadi sasa hakuna mwanamke anayeshika wadhifa wa Rais, Makamu wa Rais wala Waziri Mkuu.

Kama ilivyo kwa wabunge, nafasi za mawaziri wanawake Tanzania nazo hazizidi asilimia 50.

Hata hivyo kuna majaliwa kidogo ya mafanikio ikilinganishwa na Baraza la Mawaziri la mwaka 2005.

Wanawake wanabaki nyuma katika nafasi za juu za uamuzi



“Idadi ya mawaziri wanawake imeongezeka kutoka sita kati ya mawaziri 25 mwaka 2005 hadi kufikia mawaziri wanawake 10 kati ya 30 mwaka huu,” alisema Waziri Simba, huku kiwango hicho kikiwa ni asilimia 33 ya Baraza la Mawaziri lililoteuliwa na Rais Kikwete ambalo linamaliza muda wake Oktoba, mwaka huu.

Idadi hiyo kiasilimia ni sanjari na ile ya Kenya yenye mawaziri wanawake sita tu kati ya 18 wa Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta.

Kiwango hicho ni kidogo ukilinganisha na Rwanda ambako tovuti ya Serikali ya nchi hiyo inaonyesha kuna mawaziri wanawake 12 kati ya 31 ikiwa ni takriban asilimia 39 ya baraza lote.

Hata wakati idadi ya wanawake katika Bunge na Baraza la Mawaziri nchini ikikua kwa wastani, idadi ya wanawake katika kamati mbalimbali za Bunge siyo ya kuridhisha.

Kwa mujibu wa tovuti ya Bunge la Tanzania, kati ya kamati 18 za

Bunge ni wanawake sita tu ndiyo wanaoshikilia nafasi za uenyekiti huku wengine watatu wakiwa ni makamu wenyeviti.

Idadi hiyo ni takriban asilimia 33 kwa wenyeviti wa kamati huku kukiwa na asilimia 17 ya makamu wenyeviti.

Pamoja na idadi hiyo, baadhi ya wanaharakati, wanataaluma na wananchi wa kawaida wanabainisha kuwa ukilinganisha na ilivyokuwa Bunge la Tisa, baadhi ya wabunge wanawake wamefanya kazi kubwa ya kutetea masilahi ya umma huku wengine wakipoteka kabisa.

Hata hivyo, huenda wabunge hao wangepanya kazi kwa ufanisi zaidi iwapo mfumo wa uteuzi ungekuwa wa kidemokrasia zaidi kwa kuchaguliwa na wananchi, kama anavyoeleza Mratibu wa Umoja wa Wanawake Wanasiasa Tanzania (Ulingo), Dk Ave Maria Semakafu.

“Wabunge wanawake wamefanya kazi vizuri kwenye masuala yaliyohitaji kiwango kikubwa cha fikra hasa katika hoja zilizokuwa moto na kuleta mjadala mkubwa.

“Mafanikio hayo tuliyaona pia kwa Bunge zima siyo wanawake tu...ila ilibidi wanawake wawe huru na wenye nguvu ya kutosha ili kuwianisha nguvu za hoja na wanaume,” anasema Dk. Semakafu.

Anasema mfumo wa uteuzi wa wabunge wa viti maalumu umefanya wawakilishi hao wasijitume inavyotakiwa na wadharaulike ndani ya jamii kwa kukosa watu wa kuwawakilisha na upatikanaji wao huhusisha rushwa na kutegemea matakwa ya chama bila kuzingatia uwezo na uweledi. ▶ Uk 27

« Uk 26

Hoja hiyo inaungwa mkono na Mhadhiri wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Richard Mbunda anayesema mchango wa wabunge wanawake kiujumla haukuwa mzuri japo baadhi yao walifanya vizuri zaidi ya wanaume kama Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee.

“Wengi walifanya kazi ya chini kwa kutochangia hoja mara kwa mara au kutoa hoja binafsi. Bila shaka mfumo wetu wa viti maalumu ni mbovu usioweza kuchagua watu wenye uwezo wa kufanya kazi inavyotakiwa bungeni,” anasema Mbunda.

“Hata kwenye Baraza la Mawaziri, wanawake hawakufanya kazi kubwa sana ambayo mtu anaweza akasema imetukuka na kukumbukwa.


“Baraza hilo liliundwa kisiasa na lilionekana lina idadi kubwa ya wanawake wasio na uwezo mkubwa.”

Kwa wananchi, utendaji wa wanasiasa wanawake ulitegemea utashi na uwezo wao binafsi bungeni na katika Baraza la Mawaziri.

“Sifuatili sana Bunge, lakini mchango wa wanawake bungeni ulikuwa hafifu ukilinganisha na wanaume,” anasema Mwajuma Salum, mkazi wa Makumbusho, Jijini Dar es Salaam.

“Kitu cha msingi ni kwamba wanawake wanatakiwa wajifunze kujenga hoja kwa kufanyia utafiti michango yao kwa sababu Bunge siyo taasisi ya kisiasa tu, kuna masuala mengi ya kitaaluma yanayohitaji uelewa na taarifa za kutosha kabla mtu hajachangia mijadala kama ya bajeti na miswada ya sheria.”

Wanawake wanabaki nyuma katika nafasi za juu za uamuzi



Ushiriki hafifu wa wanawake katika nafasi za kisiasa unaonekana wazi katika mfumo wa uongozi wa vyama vya siasa nchini ambako kati ya vyama 22 vilivyopata usajili wa kudumu, ni mwanamke mmoja pekee anayeshika wadhifa wa mwenyekiti.

Taarifa ya Ofisa habari wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inaonyesha kuwa kuna makatibu wakuu watano wanawake wa vyama vya TLP, CHAUSTA, DP, Jahazi Asilia na ADC na Mwenyekiti pekee ni wa ACT-Wazalendo, Anna Mghwira. •



Wanaharakati wakiwa katika moja ya maandamano ya kudai haki za wanawake nchini.

Vyombo vya habari vyabagua wagombea wanawake

Na Shadrack Sagati



TAMWA ilitoa mafunzo kwa wahariri na waandishi wa habari kabla ya kura za maoni ndani ya vyama vya siasa kwa nia ya kuongeza kiwango na idadi ya habari za wanawake. Ingawa kuna mabadiliko kiasi jinsi habari zinavyoandikwa, bado waandishi wanahitaji kuwapa wanawake nafasi na muda wa kutangazwa

Wanawake saba walijitokeza ndani ya Chama cha Mapinduzi kuomba kugombea urais kwa tiketi ya chama hicho katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Wanawake hao ni Amina Salum Ali, Dk Mwele Malecela, Dk Asha-Rose Migiro, Ritta Ngowi, Hellen Elinawinga, Veronica Kazimoto na Monica Mbega.

Wanawake hao saba ndiyo walioonyesha nia ya kuitaka nafasi hiyo ya juu ya uongozi kwa mwaka huu, ndani ya CCM huku mmoja Anna Mghwira wa ACT - Wazalendo akiwa pekee aliyepewa fursa ya kugombea.

Kwa CCM wanawake hao walikuwa miongoni mwa makada 42 waliotangaza nia ya kugombea urais kupitia chama hicho tawala na katika mchujo wa awali walibaki watano huku wanawake wawili – Balozi Amina Salum Ali na Dk. Asha-Rose Migiro wakiingia katika kundi la tano bora. Mchujo wa tano bora ulibakisha wanawake wawili na mwanamume mmoja, Dk John Pombe Magufuli.

Hata hivyo, mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ilimteua Dk. Magufuli kupeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi wa Oktoba 2015. Dk. Magufuli naye alimteua Samia Suluhu Hassan kuwa

mgombea wake mwenza, na hivyo kuwa mara ya kwanza kwa chama hicho kuwa na mgombea mwenza mwanamke.

Katika vyama vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), Waziri Mkuu wa zamani Edward Lowassa ambaye alikihama chama chake cha CCM baada ya mchakato wa uteuzi wa mgombea na kuhamia CHADEMA, aliteuliwa kupeperusha bendera ya urais ya umoja huo. Naye alimteua Juma Duni Haji kuwa mgombea wake mwenza. Ili kupata nafasi hiyo Duni Haji alilazimika kujivua uanachama wake CUF alikokuwa makamu mwenyekiti na kujiunga na Chadema.

Magazeti mengi ya Juni yameandika habari nyingi za wanasiasa wanaume ambao walionyesha nia ya kutaka kugombea urais kama Edward Lowassa na Bernard Membe, January Makamba na Steven Wassira. Wanasiasa hao habari zao zimekuwa zikichomoza kila siku toka walipochukua fomu tofauti na wagombea wengine. ►► Uk 29

Lakini swali la msingi la kujiuliza hapa ni je, vyombo vya habari vimetoa habari za wanawake hao saba waliojitokeza na kutengeneza historia mpya nchini ikilinganishwa na wenzao wanaume?

Dk Hellen Kijo Bisimba ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, anasema vyombo vya habari havijaripoti habari za wanawake hao kwa wingi kama ilivyo kwa wanaume.

“Tuliwasikia na kuwasoma mara walipokwenda kuchukua fomu, baada ya hapo hawasikiki tena kwenye vyombo vya habari,” anasema Dk Bisimba.

Anasema vyombo vya habari havijawatendea haki wanawake hao na hiyo anasema ni kutokana na mfumo uliopo nchini wa kuwaona wanawake kama daraja la pili, hawawezi kushika nafasi hizo za juu.

“Kama utaona wanaume walionyeshwa na wake zao pale na bado wanaendelea kusikika huko wanakotafuta wadhamini, lakini naamini wanawake waliokwenda kuchukua fomu hata waume zao hawajulikani na hawasikiki kabisa,” anasema Dk Bisimba.

Mwanaharakati huyo anasema vyombo vya habari vinatakiwa kubadilika na kuwapa nafasi sawa wagombea hao badala ya kuwabagua kwa sababu tu ni wanawake.

“Bado vyombo vya habari havijachelewa, waandishi na wahariri najua wako kwenye jamii ya mfumo dume, lakini wanaweza kurekebisha hili.”

Ussu Malya kutoka Kitengo cha Wanawake cha Umoja wa Mataifa

Vyombo vya habari vyabagua wagombea wanawake



(UN Woman), anasema hajafanya utafiti wa kina kuhusu namna wanawake hao wanavyoandikwa, lakini anasema habari zao hazisikiki.

“Sikuwepo kwa siku kadhaa, sijafanya uchambuzi wa kina, lakini wanaume wanasikika zaidi kuliko wanawake,” anasema Mallya.

Dk Ayoub Rioba wa Shule ya Uandishi wa Habari na Mawasialino ya Umma (SJMC), anasema wanawake ambao wamejitokeza kutangaza nia ya urais waliandikwa na vyombo vyote vya habari, lakini hawajaandikwa mara nyingi kama ilivyo kwa baadhi ya wagombea wanaume.

“Hiyo inaeleweka kwa sababu vyombo vyote vya habari vinaandika habari kwa kuzingatia umaarufu wa mtu, hivyo nikiri kuwa wanawake hao wanne hawajaandikwa kwa wingi kama ilivyo kwa Membe (Bernard) na Lowassa (Edward),” anasema.

Anasema wagombea hao wawili wameandikwa zaidi na vyombo vya habari kutokana na kuwa na makundi ndani ya CCM na ndiyo maana wakati wanatangaza nia wameendelea kuandikwa

kwenye kurasa za mbele za magazeti na kutangazwa zaidi na radio na televisheni.

Hata hivyo, Dk Rioba anavishangaa baadhi ya vyombo vya habari kumdharau Dk Asha-rose Migiro wakati alipotangaza nia vikaandika ‘Migiro naye ajitosa kuwania urais’ jambo linaloonyesha kuwa wanamchukulia kama mtu ambaye hana nguvu na hastahili kuwania nafasi hiyo.

“Hii ilinishangaza sana inakuwaje wanamdharau Dk Migiro wakati huyu amekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Waziri wa Mambo ya Nje waseme ‘naye ajitosa kuwania urais?’ alihoji Dk Rioba na kusema kama wangeandika hivyo kwa Dk Mwele Malecela asingeshangaa maana watu wengi hawakutarajia kuwa angeingia kwenye siasa na moja kwa moja akaenda kugombea urais.

Kuhusu Amina Salum Ali Dk Rioba anasema alitarajia vyombo vya habari vimpe uzito maana amewahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha wa Zanzibar, lakini hajaandikwa inavyostahili ili watu waweze kumfahamu. ▶▶ Uk 30

Mwanahabari nguli nchini, Ndimara Tegambwage anasema wagombea urais wanawake wameandikwa baada ya kuchukua fomu za kuwania urais, lakini hawajaandikwa kwa wingi kama wanaume walipokuwa huko wanatafuta wadhamini.

Tegambwage anasema haamini kama kuna ubaguzi unaofanywa na vyombo vya habari ila yawezekana kile kilichofanywa na wanaume kusafiri na maandishi wa habari hakikufanywa na wagombea wanawake hali ambayo ilifanya wasisikike.

“Si unajua kwamba kuna wagombea wana msururu wa maandishi wa habari, yawezekana wagombea wanawake hawana hao maandishi wa habari kwenye misafara yao ndiyo maana hawasikiki,” anasema Tegambwage.

Hata hivyo, anawalaumu maandishi wa habari kuwa wamekuwa wanasubiri kuitwa kwenye matukio ya wagombea badala ya kuwatafuta ili waandike makala zao na wananchi waweze kuwafahamu kwa kina.

Lakini pia anasema, siyo rahisi kwa wanawake waliojitokeza kuandikwa sawa na wanaume waliojitokeza hasa ikizingatiwa kuwa thamani ya habari inatokana na mtu mwenyewe.

“Humu kuna majina makubwa ya watangaza nia wengine wanaambiwa ni mafisadi wanastahili kuwa jela, lakini pia wana wafuasi wengi ndani ya chama.”

Anasema wanawake waliojitokeza kuchukua fomu wengi hawana kashfa na wala hawana cha kuandikwa ambacho

Vyombo vya habari vyabagua wagombea wanawake



kinaweza kuwavutia wasomaji jambo ambalo pia anasema linawafanya wasiandikwe zaidi kama wanaume maana maandishi wamejielekeza huko.

Kwa hali hiyo, anasema wanawake wanaandikwa kama wakivifuata vyombo vya habari vyenyewe.

“Nimemwona Amina Salum Ali kaenda kwenye baadhi ya vyumba vya habari na tumeona habari zake na hawa kina Dk Mwele na Dk Migiro waende huko waweze kuandikwa.”

Anasema wanalazimika kufanya hivyo kwa kuwa vyombo vya habari vingi hapa nchini vinatafuta watu maarufu zaidi kwa lengo la kuuza magazeti yao.

“Pia posho inachangia baadhi ya wagombea kuandikwa sana na baadhi wasiandikwe sana,” anasema Tegambwage na kupendekeza kuwa kama wanataka kuwapa haki ya kuandikwa wanawake waliochukua fomu wawatume maandishi wa habari wakawahoji na badala ya kusubiri kuitwa kwenye matukio.

Anasema asasi zisizokuwa za kiserikali nazo zinajukumu la

kuhakikisha zinatoa mafunzo kwa maandishi wa habari ili kuwajengea uwezo waache kubagua wanapokuwa wanaandika habari za wagombea.

“Nawataka wahariri wa vyombo vya habari kufanya kazi bila ubaguzi wa aina yoyote ile”, anasema.

Baadhi ya watu waliohojiwa na Sauti ya Siti kuhusiana na kukosekana kwa habari za wagombea wanawake katika vyombo vya habari, walivitupia lawama vyombo hivyo kuwa vinawatenga.

Betram Athony, anasema wanawake hao hawajaandikwa kama wanavyoandikwa wanaume kwa sababu ndani ya vyombo vya habari bado kuna mfumo dume.

Anasema inaonekana kuwa wanawake hao wana nia ya dhati, lakini baadhi ya watu wanawaona kama hawawezi na wamejitokeza kuchagiza mbio hizo ili ionekane kama kuna demokrasia.

Hata vyombo vya habari vingi havitaki kupoteza muda kuandika watu ambao wanawaona kama ni wasindikizaji na wanawaona kuwa hata kwenye tano bora hawaingii kwa kile kinachoonekana kuwa hawana uwezo wa kuhimili ushindani dhidi ya wanaume”, anasema.

Athony ambaye ni Mtanzania kijana anataja sababu nyingine ya wanawake hao kutoandikwa kuwa ni kutosafiri na maandishi wa habari kama wanavyofanya wagombea wanaume. ...“Kinachotakiwa hapo ni maandishi wa habari kwenda kuwatafuta wao ila katika siku za hivi karibuni maandishi nao wameegemea kwa wagombea wanaotoa chochote.” ●



Senkoro: Serikali itoe ruzuku kwa wagombea wanawake



Anna Senkoro alikuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kugombea urais nchini Tanzania.

Na Agnes Temu

Ni miaka 54 sasa tangu Tanzania ipate uhuru wake kutoka kwa Mwingereza. Baada ya Uhuru serikali ya wakati huo ilidhamiria kukabiliana na maadui watatu, umaskini, ujinga na maradhi.

Pia, iliweka msukumo wa kipekee wa kuhakikisha inaimarisha dhana ya utawala bora ili kuwawezesha wananchi kuwa na uhuru wa kutoa maoni yao, kukusanyika na kushiriki kikamilifu katika shughuli za siasa.

Dhamira kubwa ya serikali ilikuwa kuona kuwa inatoa fursa sawa kwa raia wake na kwamba, viongozi wa kisiasa waliopewa fursa za kuongoza ni wale tu ambao walikuwa na mweleko sahihi kuhusu masilahi ya Taifa.

Ni ukweli ulio wazi kwamba rais ndiye kiongozi wa utumishi wa umma.

Yeye ni mtumishi nambari moja. Kwa miaka yote hiyo, Tanzania imekuwa katika harakati kubwa za kupambana na tatizo la usawa wa kijinsia na pia,

kwa miaka yote hiyo haijawahi kutokea nafasi hiyo ya urais ikashikwa na mwanamke.

Jitihada na matamano ya wanawake kuwania nafasi hiyo zimeendelea kujitokeza kwa kipindi chote hicho ambacho kimeshuhudia wanawake kuanzia chama tawala mpaka vyama vya upinzani wakijitokeza kwa lengo la kutaka kushika wadhifa huo.

Mwanasiasa mwanamke, Anna Senkoro ndiye aliyeanza kuchomoza hadharani kuwania nafasi hiyo. Kupitia tiketi ya chama cha upinzani cha PPT - Maendeleo, Senkoro aliidhinishwa rasmi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) kuwania urais katika uchaguzi wa mwaka 2005 na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kuwania nafasi hiyo.

Kwa mara nyingine mwaka huu tunaingia katika uchaguzi mkuu. Yeye ana uzoefu wa aina yake kuhusiana na siasa za Tanzania. ▶ Uk 32



Katika mahojiano aliyofanya na Sauti ya Siti, Senkoro anaeleza mengi aliyopitia wakati alipozunguka katika majukwaa ya kisiasa akisaka kuweka historia ya kutaka kuwa rais wa kwanza mwanamke Tanzania.

Senkoro anasema wanawake bado wanakabiliwa na changamoto nyingi zinazokwamisha ndoto zao za kuwania nafasi hiyo adhimu.

Anataja baadhi ya mambo kama mila na utamaduni kuwa ni maeneo ambayo yanaifanya safari ya mwanamke kwenda lkulu kuwa ngumu.

Anasema mfumo wa kiuchumi ambao mara zote umetawaliwa na wanaume, pia umesababisha washindwe kujitokeza katika mbio za kuwania urais.

“Wote wanaume na wanawake bado hawaamini kama mwanamke anao uwezo wa kuwa kiongozi katika Taifa hili. Wanawake wenzangu ndiyo waliokuwa wa kwanza kunikatisha tamaa.

“Walifikiri sikuwa mgombea sahihi na ndipo nilipoamua kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kuwa na fursa sawa kwa wote na hii ilichukua muda wangu mwingi wa kampeni,” anasema Senkoro.

Amelalamikia kuhusu mila potofu zinazoendelezwa na wanaume barani Afrika ambao baadhi yao wamekwenda mbali zaidi wakiamini kuwa ni jambo la laana kwa mwanamke kusimama mbele ya wanaume na kuzungumza jambo lolote.

Senkoro: Serikali itoe ruzuku kwa wagombea wanawake



“Nilipata upinzani mkubwa katika maeneo ya kusini na Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Mara ambako dhana hii imetawala.

“Kwa vile mila hizi zimeota mizizi huku zikiendelea kumpendelea mwanamke, nililazimika kusimamisha kampeni zangu kwa muda ili kuendesha semina kuhusu suala la usawa wa kijinsia.

“Niliwaelimisha kutambua thamani ya mwanamke na umuhimu wa kuwa na kiongozi mwanamke. Baada ya kazi kubwa ya kuwaelimisha iliyotumia muda mwingi hatimaye baadaye wazee walinikubalia ili niendeshe mikutano ya hadhara. Yaani nashindwa kabisa kueleza jinsi kazi hii ilivyokuwa na changamoto nyingi,” anasema Senkoro.

Anasema hata baadhi ya wanawake walijitokeza na kumpinga wakimwelezea kuwa

wakati wao wa kuongoza nchi ulikuwa bado haujafika.

Hata hivyo, Senkoro anasema alipata msaada mkubwa kutoka kwa Mkurugenzi wa ITV/Radio One, Joyce Mhaviile aliyekubali kumpa muda katika vituo vyake.

“Alinisaidia sana kwani kila siku alinipatia muda wa saa moja katika kituo cha ITV bila malipo yoyote. Namshukuru sana Mhaviile,” anasema Senkoro.

Suala la ukosefu wa vitendea kazi lilikuwa ni changamoto nyingine kubwa iliyomfanya mwanasiasa huyo kujikuta akikwama.

Hata hivyo, anasema chama chake cha PPT- Maendeleo kilikuwa hakipati ruzuku yoyote kutoka serikalini jambo lililofanya kukosekana kwa fedha za kugharamia kampeni zake.

“Familia yangu ilinisaidia sana. Mara zote tulitumia kile kidogo tulichokuwa nacho ndani ya familia yetu. Mume wangu alijitahidi kila alivyoweza ili kufanikisha kampeni zangu,” anasema Senkoro.

Anasema kukosekana kwa fursa sawa na ukandamizaji ndani ya chama tawala ndiko kulikomfanya aachane na chama hicho na hatimaye kutimkia upinzani.

“Ni vigumu sana kuweza kushika nafasi za uongozi ndani ya chama tawala. Viongozi wanawake wanawakandamiza wanawake wenzao ili waendeleo kusalia kwenye nyadhifa hizo,” anasema Senkoro.

Uwezekano wa Tanzania kupata Makamu wa Rais mwanamke



Mgombea mwenza wa CCM Samia Suluhu Hassan akirejesha fomu za kugombea makamu mwenyekiti wa Bunge la Katiba mjini Dodoma. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa zamani wa TAMWA, Valerie Msoka ambaye pia alikuwa mjumbe wa Bunge hilo.

Na Deogratias Mushi

Kuna uwezekano mkubwa kwa Tanzania kupata Makamu wa Rais mwanamke wa kwanza katika historia iwapo Watanzania wataridhia kukirudisha madarakani Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichomteua Bi. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea mwenza wa Dk. John Pombe Magufuli

Wawili hao wameteuliwa na chama hicho kupeperusha bendera yake katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 25, mwaka huu.

Kwa kumteua Samia (55), CCM inaonekana imesikia kilio cha wadau wa masuala ya jinsia. Wadau hao wamekuwa wakipiga kelele kudai misingi na mifumo ya uteuzi wa viongozi katika ngazi ya juu ya uamuzi iwe na

usawa wa kijinsia.

Madai yao ni kuwa, kama rais aliyechaguliwa atakuwa mwanamume, makamu wake au waziri mkuu awe mwanamke kwa lengo la kutaka kufikiwa kwa lengo la usawa wa kijinsia wa 50 kwa 50 katika vyombo vya utoaji wa uamuzi.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Valerie Msoka anasema chama hicho kimeendelea kufanya kazi ya utetezi wa kijinsia ili kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi za juu za utoaji wa uamuzi.

"Tunasema kama rais ni mwanamume, waziri mkuu au makamu wa rais anapaswa kuwa mwanamke. Hii ni njia pekee ya kuleta usawa katika uwakilishi," alisema Msoka katika mafunzo yaliyolenga usawa wa kijinsia yaliyotolewa kwa wahariri wa

vyombo mbalimbali vya habari yaliyofanyika Juni, 2015.

Kauli hiyo ya Msoka ina maana kuwa, iwapo ikatokea CCM ikashinda, Samia ambaye aliteuliwa na chama chake kuwa mgombea mwenza Julai 12, basi kwa mara ya kwanza Tanzania itaandika historia mpya kwa wanawake kuanza kushika nafasi kubwa katika ngazi ya urais. Wakati idadi ya wanawake ni takribani asilimia 51 ya Watanzania wote, haijawahi kuwa na mwanamke kiongozi katika ngazi ya urais, makamu wa rais wala katika nafasi ya waziri mkuu.

Kabla ya mwaka 2000, Samia alikuwa mwanaharakati ambaye hakuwa na nia ya kuingia kwenye siasa.

Katika kipindi cha miaka 15 amepanda hadi kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza wa Dk. Magufuli. ►► Uk 34

Hatua hii imetengeneza njia kwa wanawake zaidi kupatiwa nafasi ya kushika nafasi za juu katika ngazi ya kisiasa ya utoaji uamuzi nchini.

Mwanasiasa huyo kwa sasa ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya muungano.

Samia anasema uteuzi wake ni mwanzo wa safari aliyoiita kuwa ni ngumu na wala siyo zawadi katika sahani ya dhahabu kama wanavyosema baadhi ya watu alioidai kuwa bado wanatawaliwa na mfumo dume kifikra.

Anasema nafasi anayotarajia kuishika, inabeba majukumu mengi, hivyo anahitaji kujiandaa kikamilifu kwa msaada wa Mungu na Watanzania wote bila kujali jinsia, rangi, sura wala kabila.

“Watu wanasema nimeukata, lakini katika uhalisia, nafasi kama hiyo inahitaji kujitoka kwa kiasi kikubwa ili kuhakikisha kuwa natumikia Taifa kwa moyo na kwa uaminifu,” aliwaambia wapigakura wa jimbo lake la Makunduchi, Zanzibar, hivi karibuni.

Mgombea mwenza huyo ambaye alikuwa pia Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, ametofautiana na wakazi wa Makunduchi ambao walimpongeza, kwa kusema kuwa “ameukata”.

Anasema akiwandiye mwanamke wa kwanza nchini kuteuliwa kuwa mgombea mwenza katika kiti cha urais kwa tiketi ya CCM, atajitahidi kuona haki inatendeka hasa katika ngazi za uamuzi.

Uwezekano wa Tanzania kupata Makamu wa Rais mwanamke



“Tukijaliwa chama chetu kikaendelea kushika dola, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kuona haki inatendeka kwa ajili ya ustawi wa jamii na maendeleo kwa Taifa,” alisisitiza Samia.

Anasema kipaumbele chake kikubwa ni maendeleo ya wanawake na watoto kwa sababu anaamini kuwa unapoyapatia uwezo makundi hayo mawili, jamii inapata maendeleo ya haraka.

Mwanamama huyo anasema anaguswa na ukweli kwamba bado kuna maeneo mengi nchini ambayo yanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama, huduma bora ya afya na elimu bora, jambo linalohitaji watu makini kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu.

Samia anahusisha pia kupanda kwake chati katika ngazi ya siasa kuwa ni pamoja na kujiamini, utendaji kazi mzuri na uthubutu wake na ndiyo maana chama chake kupitia kwa mgombea urais Dk. Magufuli wamemwamini na kumpa kazi hiyo ya kupeperusha bendera katika nafasi ya ugombea mwenza.

Hata hivyo, anasema siyo rahisi kuhama kutoka katika uanaharakati na kuingia kwenye siasa kutokana na viongozi wengi serikalini kuwa na mtizamo hasi juu ya uanaharakati.

Huyo ndiye Samia ambaye hakuna shaka kuwa jina lake limeshaingia katika vitabu vya historia ya Tanzania kuwa ni mwanamke ambaye alibeba jukumu kubwa wakati wa mchakato wa kuandika Katiba Mpya Inayopendekezwa.

Akiwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, Samia alifanya kazi kwa karibu na aliyewahi kuwa waziri wa siku nyingi nchini, Samuel Sitta, ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti wa Bunge hilo.

“Nikiwa nimewahi kufanya kazi kama mwanaharakati katika ngazi ya jamii na kushuhudia kwa macho yangu jinsi watu wanavyopata shida kila siku; niliona ni wakati muafaka wa kujiunga na siasa na kuleta mabadiliko katika jamii,” alisema Samia alipozungumzia safari yake ya uanasiasa alipozungumza na Sauti ya Siti ofisini kwake mjini Dodoma.

Samia anashahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Southern Hampshire nchini Marekani akiwa amebobea katika masuala ya Uchumi. ●

Anasema aliamua kuwania uongozi katika uchaguzi wa 2005 ili kuwakwamua Watanzania katika hali ya umaskini.

“Maisha ni magumu sana kwa Watanzania. Nchi hii ina kila aina ya rasilimali inayohitajika ili iwe tajiri, inashangaza bado ni maskini.

“Tunayo mito, maziwa, bahari na rasilimali nyingine nyingi. Hatukustahili kuendelea kuwa maskini,” anasema Senkoro.

Kudhihirisha kwamba Watanzania wanaweza kuondokana na tatizo la umaskini, Senkoro ameanza kujishughulisha na watoto wa mitaani ambao wamekuwa wakiishi katika mazingira hatarishi. “Nimeanzisha vituo viwili kwa watoto wanaoishi kwenye maisha magumu, kimoja kipo Tanga na kingine kipo Moshi. Tunaweza kufanya vitu kama hivi nchi nzima na kuwapatia stadi za maisha ili waendeleo na maisha yao hapo baadaye,” anasema Senkoro.

Alipoulizwa kama anadhani mwanamke anaweza kuja kuwa rais wa Tanzania, Senkoro anasema “Kuna wanawake wengi wenye uwezo wa kuwa marais lakini bado hawajataka kujitokeza.

Wanawake kama Sophia Simba na Anne Makinda ni watu wenye sifa zote za kuwania nafasi hiyo,” anasema.

Anasema wanawake wote waliochukua fomu kupitia CCM kuwania nafasi hiyo bado wamekosa sifa kwa vile hawana uzoefu wa kutosha na kwamba, baadhi yao hawana uhusiano

Senkoro: Serikali itoe ruzuku kwa wagombea wanawake



wa karibu na raia wa kawaida kutokana na muda wao mwingi kuwa nje ya nchi.

Anasitiza kuwa ili mwanamke ashinde nafasi ya urais, Serikali

inapaswa kuanzisha mfumo mpya wa kuwapatia ruzuku wale wanaowania nafasi mbalimbali kama udiwani, ubunge na urais.

Senkoro anasema bado kuna haja kwa mashirika ya kiraia kikiwamo Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kutoa elimu ya usawa wa kijinsia na kuanzisha mijadala ya mara kwa mara itakayoibua masuala mengi ambayo baadaye, yatasaidia kuwajengea uwezo wanasisa hao wanawake.

Akizungumzia kuhusu viti maalumu kwa wanawake, Senkoro anasema wakati umefika kwa wanawake kwenda kugombea katika majimbo ya uwakilishi na siyo kuendelea kutegemea upendeleo.

Akihitimisha maelezo yake, Senkoro anasema: “Nimerejea CCM na sasa ni kada wa kudumu wa chama hiki. Ninalo jukumu la kuitumikia jamii na katika kipindi cha miaka 10 ijayo nitawania tena nafasi ya urais.” ●

1. Katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995 idadi ya wanawake bungeni ilikuwa asilimia 16 tu. Kati ya majimbo 232, wanawake waliweza kushinda katika majimbo 8 tu.
2. Idadi ya wanawake bungeni iliongezeka kutoka asilimia 16 mwaka 1995 hadi asilimia 36 mwaka 2015
3. Idadi ya wanawake bungeni imeongezeka kutoka 62 kati ya wabunge 288 mwaka 2005 hadi 127 kati ya wabunge 357 mwaka 2015.